ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Nane – Tarehe 28 Januari, 2011

Kikao kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 85

Utunzaji wa Gari za Serikali

Mhe. Fatma Mbarouk Said - Aliuliza:-

Gari nyingi za Serikali zinakufa haraka kwa sababu ya kukosa matengenezo na kutunzwa ipasavyo.

(a) Je, Mhe. Waziri wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha gari za Serikali zinatunzwa ipasavyo ikiwa ni pamoja na kufanyiwa matengenezo ili kuepusha kufa haraka kwa gari hizi.

(b) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba kutoangaliwa na kupasishwa kwa gari za Serikali kunachangia kufa haraka kwa gari hizi na kusababisha ajali za mara kwa mara barabarani.

(c) Je, wizara haifahamu kwamba kitendo cha kutopasishwa kwa gari za Serikali kunaiigizia hasara Serikali ikiwa ni pamoja na kufa na kuchakaa haraka kwa gari za Serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 85 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba gari nyingi za Serikali zinakufa haraka kwa sababu ya kukosa matengenezo na kutunzwa ipasavyo ikiwa ni pamoja na kufanyiwa matengenezo (*maintenance*) kwa wakati.

(a) Kwa ajili ya kuhakikisha kwamba magari yote ya Serikali yanatunzwa ipasavyo na yanafanyiwa matengenezo kwa wakati wizara yangu inatoa wito kwa zote za serikali kufuata utaratibu wa sheria juu ya

matumizi na matengenezo ya magari ya serikali kama ilivyoelezwa katika sheria Nam. 13 ya mwaka 2004. Ni vyema utaratibu huo ukazingatiwa na kuchukuliwa hatua za kutekelezwa.

(b) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kutoangaliwa na kupasishwa kwa gari za serikali kunachangia kufa haraka kwa gari hizi kwa sababu ninaelewa kwamba ili chombo chochote kiweze kudumu lazima kiwe katika uangalizi bora na kufanyiwa matengenezo kila inapobidi (*maintenance and repair*). Aidha, napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba bado takwimu zetu hazionesha kwamba magari ya serikali pamoja na hali tuliyoieleza hapo juu kuwa ni kichecheo kikubwa cha ajali nyingi hapa nchini.

(c) Wizara yangu inafahamu kwamba kitendo cha kutokupasishwa kwa gari za Serikali kunaiingizia hasara Serikali ikiwa pamoja na kufa na kuchakaa kwa gari hizo haraka.

Mhe. Spika, napenda kutoa wito wangu kwa taasisi zote za serikali kukubaliana na matakwa ya sheria ili kuona utekelezaji wa sheria hiyo unafanyika ili kuokoa fedha nyingi za walipa kodi wa nchi hii kwa ununuzi wa magari mapya. Ni kweli serikali inalazimika kununua magari mapya ili kufidia magari yaliyoharibika kwa ajili ya viongozi na watendaji kuweza kuwasaidia waweze kufanikisha majukumu yao ya kiutendaji.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, pamoja na majibu fasaha ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa uchakavu wa magari unachangiwa sio tu na kutokupasishwa na matunzo, pia na matumizi mabaya ya magari ya serikali ambayo limekuwa jambo lilozoeleka sana katika nchi yetu. Pia imezoeleka kuyaona magari ya serikali yakitembea hadi saa sita za usiku kwa shughuli ambazo sio za kiserikali.

Je, ni lini Mhe. Naibu Waziri katika kuihami nchi yetu na matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi ambao wengi wao ni masikini wakutupwa serikali itapiga marufuku utumiaji mbovu wa magari ya serikali ili kuhakikisha tunazitunza fedha zitolewazo na zitumike zaidi kwa shughuli za maendeleo ya wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika jibu mama nilisema kwamba tunaiomba serikali na taasisi zote zinazohusika zizingatie maelekezo yaliyotolewa na sheria Nam. 13 ya mwaka 2004, sheria hii imetoa muongozo kwa maelezo yote juu ya utaratibu wa kuendesha magari, utaratibu wa matengenezo, utaratibu wa kutunza na taratibu zote zinazohusiana na uendeshaji wa magari. Naomba tena nitoe wito wangu kwa taaisisi za serikali tuzingatie sana matakwa na masharti yaliyoelezwa katika sheria hii.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika kutengeneza magari kwa nia nzuri serikali ilijenga Karakana kwa ajili ya magari ya serikali yote kutengenezwa katika Karakana hiyo. Lakini tunaziona gari za serikali zikitengenezwa sehemu ovyo ovyo, suala ambalo linasababisha aidha serikali kutumia fedha nyingi au kuibiwa kwa ajili ya matenengenezo ya nje.

Je, ni lini hasa serikali itaweka mkakati wa kutengeneza gari katika Karakana ya serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli utaratibu ulielezwa katika sheria Nam. 13 ya mwaka 2004 inazitaka taasisi zote za serikali kufanya matengenezo katika Karakana kuu ya serikali. Lakini sheria hiyo hiyo imetoa fursa na ruhusa kwa Mhe. Waziri kutoa maelekezo yakufanya matengenezo gari hizo nje ya Karakana ya serikali pale panapokuwa kuna haja. Kama tunavyotambua magari yetu mengi hivi sasa yako katika mfumo wa Toyota, Karakana yetu iko nyuma katika mfumo huo wa matengenezo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri aliyetangulia alitoa ruhusa ya kwamba magari yale yaliyotengenezwa katika mfumo wa Toyota yakatengenezwe gereji ya Buda, alitoa maelekezo hayo kwa mujibu wa sheria na hayakuwa makosa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kwamba hadi sasa pamoja na ruhusa iliyotolewa na Mhe. Waziri aliyepita lakini Karakana yetu kwa magari ambayo sio ya Toyota ina uwezo mkubwa wa kuyatengeneza na hadi sasa kumbukumbu zetu zinaonesha kwamba wizara na taasisi zifuatazo ndizo pekee ambazo zimepeleka magari yao kwenye Karakana yetu.

1. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano likiwemo Shirika lake la Bandari.
2. State University of Zanzibar (SUZA)
3. ZRB
4. Idara ya Vitambulisho
5. Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo
6. Shirika la Umeme la Zanzibar

Mhe. Spika, natoa wito kwa magari ambayo sio ya Toyota kwa wizara zilizobakia waje katika Karakana yetu na yatatengenezwa vizuri zaidi kuliko yanavyotengenezwa katika Karakana za nje ambazo baadhi ya Karakana za nje tumegundua kwamba hayo hayo magari ya serikali yanayopelekwa basi

Karakana hizo za nje hupeleka magari hayo hayo kwenye Karakana yetu. Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam. 93

Utoaji wa Viyoo vya Kiza "*Tinted*" kwenye Gari

Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak - Aliuliza:-

Hivi karibuni Jeshi la Polisi la Zanzibar limeagiza kutolewa viyoo vya kiza "*tinted*" kwenye magari ya wananchi.

(a) Je, Mhe. Waziri kuweka gari viyoo vya kiza "*tinted*" ni kinyume na sheria gani ya Zanzibar na kifungu cha ngapi cha sheria hiyo.

(b) Kama Sheria za Zanzibar hazizungumzii chochote kuhusiana na kadhia hii mnawaambia nini wamiliki wote wa gari zilizotolewa viyoo vya kiza "*tinted*" tarehe 23/12/2010 katika Uwanja wa Ijitmai – Magogoni Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 93 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli hivi karibuni Jeshi la Polisi la Zanzibar limeagiza kutolewa vioo vya kiza "*tinted*" kwenye magari yote yaliyopatikana na uwekaji wa vioo hivyo, kuweka gari vioo vya kiza "*tinted*" ni kinyume na Sheria ya Usafiri Barabarani Nam. 7 ya mwaka 2003 kifungu cha 9(h) na kifungu cha 37b (I) cha Kanuni ya Cap 135 ya mwaka 1955.

b) Mhe. Spika, Sheria ya Zanzibar ya Usafiri Barabarani imezungumzia vya kutosha kuhusiana na suala zima la uwekaji wa vioo vya kiza katika magari. Suala la uwekaji wa vioo vya kiza katika magari ni kinyume na sheria kama nilivyoeleza hapo awali.

Aidha, naomba kutoa wito kwa wamiliki wote wa magari yaliyowekwa vioo hivyo vya kiza kwamba kitendo hicho ni kinyume na sheria na hivyo naomba wamiliki hao waviondowe vioo hivyo ili kuepuka ajali na kutimiza masharti yaliyowekwa

kwa mujibu wa sheria husika kwa madhumuni ya kumsaidia kila mtumiaji wa barabara yetu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa kuweka vioo vya kiza katika magari ni kinyume cha sheria kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri.

Je, kwa nini serikali inaruhusu bidhaa hii kuingizwa nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, uwekaji wa vioo vya kiza katika magari ni marufuku kwa mujibu wa sheria kwa maeneo maalum. Uwekaji huu wa marufuku ni kwa kioo cha mbele, vioo vya pembeni na kioo cha nyuma, lakini kwa magari ya abiria ni marufuku kwa maeneo yote.

Mhe. Spika, uingiaji wa bidhaa hii una njia nyingi, yapo magari ambayo tokea yanapotengenzwa huwa yanakuja yamewekwa vioo vya kiza na yanapofika hapa uingiaji huo huwa hatuna uwezo wa kuuzuia isipokuwa gari hiyo isitembee barabarani ili taasisi husika waliondowe tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, serikali haikupiga marufuku biashara hii kwa sababu *tinted* sio lazima iweko kwenye magari tu. Ni kwamba Afisi zetu nyingi za serikali wanazojenga zile sehemu ambazo hawatakiwi walioko nje kuona ndani basi zile *film* zinazofanya kioo kiwe *tinted* zinatumika. Kwa hivyo, serikali haikuweza kwa sababu sio matumizi pekee ya magari ambayo yanatumia hii *tinted*. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ndogo pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa ni kosa kisheria gari kuwekwa *tinted* na kwa kuwa gari nyingi za viongozi wakuu nazo zina *tinted*.

Je, ni nini msimamo wa serikali katika hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika jibu mama tulitoa wito kwa wamiliki wote wa magari kama kuna magari ya viongozi naomba tunawaomba wito huo wautekeleze na wao waondoe *tinted* hizo.

Nam. 41

Tatizo la Kutuwama maji Katika Gati ya Mkoani

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kutuama kwa maji katika gati ya Mkoani limezumgumzwa na kupigiwa kelele muda mrefu bila ya kupatiwa ufumbuzi unaofaa.

(a) Je, Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kwamba tatizo hili linaathiri harakati za kupanda na kushuka kwa abiria katika vyombo vinavyofika hapo pamoja na uteremshaji na upakizi wa mizigo.

(b) Je, wizara ina msimamo na mipango gani ya kuondosha tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 41 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba tatizo la kutuama kwa maji katika bandari ya Mkoani linaleta usumbufu wakati abiria wanapopanda na kushuka katika vyombo vinavyofika hapo pamoja na uteremshaji na upakizi wa mizigo hasa wakati wa mvua.

(b) Kuhusu mipango ya kuondosha tatizo hilo, wizara yangu kupitia Shirika la Bandari ina mpango wa kuifanyia matengenezo sehemu hiyo inayotuama maji katika mwaka huu wa fedha 2011. Matengenezo hayo yanatarajiwa kuanza katikati ya mwaka baada ya kumalizika kipindi cha mvua cha masika na kupatikana kwa vifaa vitakavyotumika katika kazi hiyo. Aidha, kazi ya matengenezo ya sehemu hiyo inayotuama maji inatarajiwa kuchukua miezi 3 kukamilika kwa ujenzi wa awamu kwa awamu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwanza masikio yangu kidogo yalipotea nilisikia njia au barabara lakini mimi niliuliza gati ya mkoani. Sijui jibu lilikuwa ni barabara au gati.

Mhe. Spika: Mheshimiwa jibu lilikuwa ni bandari ya Mkoani.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, baada ya masahihisho yangu sasa naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Kwanza nataka nitumie fursa hii kwa ruhusa yako Mhe. Spika, kuwapongeza sana wafanyakazi wa bandari ya Mkoani kwa jitihada zao wanazochukua kuhakikisha abiria wanapanda kwa usalama katika vyombo. Hii imekuja baada ya sisi Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kufuatilia bandarini hapo. Mhe. Spika, lakini jitihada ya wafanyakazi hawa inaangushwa sana na kutuama kwa maji katika bandari hii kwa sababu magari na abiria wanaozongana katika njia nyembamba iliyobaki baada ya maji kuchukua nafasi yake.

a) Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kuendelea kuiachia hali ile inahatarisha zaidi upandaji wa abiria katika vyombo hasa ukizingatia jibu lake aliposema kwamba wataishughulikia baada ya mvua kumaliza.

b) Mhe. Spika, pale gatini pakituama maji kutokana na uteremshaji na upakizi wa mizigo tofauti na ujaji wa magari ya aina mbali mbali huwa kunafanya tope na utelezi. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba sasa anahatarisha maisha ya watu zaidi kuliko ambavyo angetarajia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika jibu mama tulikubaliana tatizo la kutuama kwa maji, lakini tumesema kwamba tutajenga kati kati ya mwaka huu 2011. Mhe. Spika, lakini kuhusu maji yanayotuama tumeandaa utaratibu mzuri wa kutafuta *pump* ili yanapotuama tuweze kuyaondosha kwa haraka kunusuru hiyo hali ya watu kupata usumbufu wakati wa kupanda na ushushaji wa mizigo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza niishukuru Kamati yake kwa kufanya juhudi hadi kamati yenyewe ikaridhika kwamba wafanyakazi wale wanastahiki pongezi. Lakini jengine ni kwamba suala la kutuama kwa maji ni suala la muda mrefu, lakini ni jana tu Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Bandari walikubali na wakaidhinisha zaidi ya shilingi milioni mia moja kwa ajili ya matengenezo yote yanayotakiwa ili maji yasituame tena pale.

Kwa hivyo, namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwa nini inafanywa baada ya mvua ya Masika ni kwa sababu tunataka tufanye kazi ya uhakika kwani vipimo ambavyo tumevipata ni kwa Masika yaliyopita, na imefika karibu mwaka mzima mpaka Masika haya. Kwa hivyo, hatukupenda kufanya marekebisho kabla ya Masika kumbe vile katika mwaka huu mwengine wa ziada kuna *deflation* iliyoongezeka. Kama alivyosema Naibu Waziri wangu ni kwamba ili usumbufu huu usiendelee tumenunua *submersible* ndogo ili maji yakituama pale kiasi ambacho yanawezwa yakanyonywa kuingizwa baharini utaratibu huo

ufanyike. Kwa hivyo, hatutegemei Masika haya makubwa baada ya hapo kwamba suala hili litakuwa lina tatizo tena. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kumbukumbu zangu zinavyonambia ni kuwa zamani gati ile ilichelewa kutengenezwa kwa sababu tuliambiwa mpaka iwe haididimii tena.

a) Je, hali hiyo imeshafikia.

b) Katika matengenezo ya gati ile tuliambiwa siku za nyuma kuwa hata huku ambako meli zinafunga gati mawe kwa namna yalivyowekwa tayari yameshachimbuka na yanahatarisha usalama wa gati ile. Mhe. Spika, sijui katika shilingi hizo milioni mia moja ni pamoja na matengenezo hayo.

c) Bandari ya Mkoani imetangazwa kuwa ni mlango wa kimataifa wa kuingilia vyombo. Je, kuna utaratibu wowote wa kuikuza zaidi ya ilivyo ili iweze kukidhi huduma hizo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, athari iliyotokea na ambayo tunaizungumzia sasa hivi imesababishwa na mambo mengi, lakini kubwa kuliko yote ni kwamba kudidimia kwa ile bandari sehemu ile ya kati kati ilitokana na ujenzi wenyewe. Mhe. Spika, bandari ile ina urefu na upana na kwa sura ni *rectangle* mote ambamo ni pembeni mwa bandari ile mmejengwa kwa kuta za zege na vyuma, lakini kati kati yake mme kumejazwa mawe yaliyofungwa kwenye nyavu yakawekwa pale.

Kwa sababu mawe yale kati kati ya jiwe na jiwe kunakuwa na nafasi na kutokana na mizigo inayokwenda pale ile nafasi ambayo inajazwa na hewa na mchanga huwa inakwenda chini. Kwa hivyo, inafika mahali kwamba ile baraza iliyokwa juu panakuwa na nafasi baina ya mawe yaliyowekwa na ile baraza iliyowekwa ya zege. Nafasi ile kwa sababu ni tupu inabidi na baraza yenyewe inabonyea lakini haina nyufa. Kwa hivyo, tunachotaka kufanya pale ni kukata ile sehemu kuijaza nafasi halafu kuweka *layer* nyengine.

Mhe. Spika, ni kwamba jengine anasema kuwa sasa hivi kuna mawe yamewekwa na kweli mawe yale yanateremka kwa sababu ya vyombo vyenyewe vinavyofunga gati kunakuwa na *propeller* wakati meli inaondoka au inafika na kuzima yale yanakuwa na nguvu kubwa. Kwa hivyo, yanapiga katika mawe yale na mawe ndio yanateremka. Mhe. Spika, ni kwamba tunafanya utaratibu huu ni mwaka wa pili kila yanapoteremka mawe yale huwa

tunayajaza. Kwa hivyo, hii milioni mia moja haihusiani kabisa na matengenezo ya mawe yale yanayoteremka.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba bandari hii waliambiwa kuwa ni mlango, mimi nasema tena ni mlango kweli na tatizo lililopo kwa nini meli nyengine ama kutoka Dubai au kutoka popote haziendi pale moja kwa moja kuteremsha mizigo. Ni kwa sababu hatujapata vifaa vya kuteremshia na kupakilia mizigo hiyo ambayo inatoka kwenye meli za kigeni. Endapo vitu hivyo vitapatikana naamini sio muda mrefu miongoni mwa vifaa ambavyo vimeagizwa ni *crane* moja kwa ajili ya Mkoani ambayo itaweza kupakua makontena ya futi 20 na 40 na kupakia makontena mengine yatakayokuwepo pale. Kwa hivyo, Mhe. Spika, haya ndio majibu ambayo ningeweza kumpa Mhe. Mwakilishi nakushukuru sana.

Nam. 72

Uajiri wa Walimu Wapya

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa walimu katika skuli zetu nchini. Kwa kuwa kuna idadi kubwa ya wahitimu wa mafunzo ya ualimu wa Skuli za Msingi (*Primary*) waliomaliza mafunzo yao ya Ualimu tokea mwaka 2008, ambao hawajaajiriwa mpaka leo.

Je, Wahitimu hao wataajiriwa lini.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kwamba baadhi ya skuli zetu zina upungufu wa walimu hasa wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza. Pia wapo baadhi ya wahitimu wa mafunzo ya ualimu kwa skuli za msingi ambao hawajaajiriwa tokea walipomaliza masomo yao mwaka 2007. Katika kukabiliana na upungufu huo katika mwaka 2009/2010 waliajiriwa walimu 500 wa skuli za msingi kwa ajili ya kufundisha katika skuli za Mkoa wa Kaskazini Unguja, Wilaya ya Micheweni na Mkoani Pemba ndizo zilizokuwa na upungufu mkubwa wa walimu.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 wizara yangu imeendelea kuajiri walimu waliomaliza mafunzo ya shahada za walimu na hadi leo tumeshaajiri jumla ya

walimu 116, kati yao walimu 78 ni skuli za Unguja na 38 kwa skuli za Pemba. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 wizara yangu inatarajia kuajiri baadhi ya walimu wa kufundisha skuli za msingi kwa kupunguza upungufu katika masomo ya sayansi na hesabu wakati hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Spika, napenda kutoa wito kwa walimu wenye vyeti vya ualimu ambao hawajaajiriwa wajiendeleze kwa masomo ili waweze kujiunga na mafunzo ya stashahada ya ualimu kwani mahitaji ya walimu wa cheti yamepungua sana.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, ni kwamba Mhe. Waziri amekiri kuwa upungufu wa walimu katika skuli za msingi na sekondari bado upo.

Mhe. Spika, kwa kuwa jengo lolote ili liwe madhubuti linahitaji msingi uliokuwa madhubuti vile vile. Kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imewagawa walimu katika makundi mawili, kundi la wataalamu na wasiokuwa wataalamu. Walimu wataalamu kwa asilimia kubwa wanasomesha katika skuli za sekondari, na wale wengine wanasomesha skuli za msingi na kwa vile wizara imeanzisha masomo ya diploma ya msingi lakini wahitimu wizara huwapangia kufundisha kule kule skuli za sekondari.

a) Je, mtindo huu ukindelea huhisi kwamba unakosesha nguvu skuli zetu za msingi.

b) Je, mtindo huu utaendelea mpaka lini.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi ni kwamba tatizo lilioko katika maskuli ni walimu wa Sayansi, Hisabati na Kiingereza kwa bahati inatokezea hawa walimu ambao waliofundishwa kwa diploma ya msingi wanao uwezo wa kusomesha masomo hayo kwa hivyo mwalimu huwa anawapangia wakasaidie katika sehemu zile kwa sababu tuna upungufu mkubwa wa walimu wa Sayansi.

Mhe. Spika, kwa hiyo mtindo huu sio kama utaendelea muda wote, Mhe. Spika, tunashukuru sana kwamba safari hii katika matokeo ya darasa la 12 wanafunzi wengi wamepasi masomo ya Sayansi. Kwa hivyo, tunategemea tutawaendeleza wale ili waweze kuziba lile pengo la kufundisha Sayansi katika skuli zetu hizi Mwenyezi Mungu akipenda. Kwa hivyo, hautaendelea kwa muda wote *inshaallah*.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali nyongeza. Mhe. Spika, mbali na kufanya kazi

ya ulinzi na usalama kwa Vikosi vyetu vya Jeshi la Wananchi Tanzania lakini pia jeshi limekuwa mstari wa mbele kutoa huduma kama elimu na afya.

Mhe. Spika, ni kwamba nachukua nafasi hii kulipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwenye kambi yake ya Alhamis Cap Pemba kwa kuamua kuanzisha skuli ya kisasa, nzuri na bora.

a) Kwa kuwa skuli hiyo ina wanafunzi wanawake na wanaume, na skuli hiyo haina mwalimu mwanamke ni lini wizara itapeleka mwalimu mwanamke kwenye skuli hiyo.

b) Ni lini wizara itamuajiri mwalimu mwenye sifa ya diploma aliyekuwa eneo la Mtangani Kiwani kusomesha skulini hapo kwa sababu kuna upungufu wa walimu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, suala hilo ndio kwanza naanza kulipata hapa na kwa kuwa analileta liwe kama ombi ili tuweze kulishughulikia suala hilo na tuwasaidie wapate mwalimu mwanamke. Vile vile ni kwamba sisi tunaajiri walimu waliokwishafika katika hatua hizo kwenye masomo ya Sayansi. Kwa hivyo, kama yupo tunamtaka.

Mhe. Spika, napenda kutoa taarifa kwamba tuna tatizo la walimu Pemba sana kuliko Unguja nasikitika kusema kuna mwalimu mmoja alikuwa ana diploma ni mwalimu mzuri wa Sayansi alikuja kwa ajili ya kuomba kazi maana hajaajiriwa muda mrefu, kumbe tatizo lake sio kwamba hajaajiriwa ni kwamba tatizo lake hataki kwenda Pemba.

Mhe. Spika, tukampa barua hapa moja kwa moja kwamba aende Pemba akasomesha akafika kule apeleke kwa Afisa Mdhamini tu aajiriwe, basi ile barua akaichana akasema bora nikae hapa hapa niwe sina kazi, jambo kama hilo linasikitisha sana. Mhe. Spika, naomba tuwe tunawashawishi watu wetu kufanya kazi popote kama wanavyosaini mikataba yao.

Nam. 6

Ajira za Walimu

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Pamoja na juhudi kubwa za Serikali na Wizara ya Elimu za kusomesha walimu na kuwaajiri walimu hao hasa katika Mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja na Pemba.

(a) Wizara ina mipango gani ya kuhakikisha kuwa wahitimu wa mafunzo ya ualimu kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi nao wanapata fursa ya kuajiriwa kwa wingi kama wanavyoajiriwa wahitimu wa mikoa mingine ya Zanzibar.

(b) Wizara ina mpango gani katika kujaribu kuhakikisha kuwa skuli nyingi za binafsi zinazofunguliwa hapa Zanzibar, zinaajiri walimu kutoka hapa hapa Zanzibar badala ya utaratibu wa sasa wa kuajiri walimu kutoka nje ya Zanzibar, kwa lengo la kupunguza tatizo la ajira kwa wahitimu wa mafunzo ya ualimu wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 kama ifuatavyo:
Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:

Ni kweli Mhe. Spika, wizara inaendelea kutoa mafunzo ya ualimu na wahitimu wa mafunzo hayo huajiriwa kufundisha katika skuli mbali mbali za Unguja na Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 wizara iliwaajiri walimu 500 waliohitimu mafunzo ya cheti cha ualimu na kupangiwa kazi katika skuli za Mkoa wa Kaskazini Unguja na skuli za Wilaya ya Micheweni na Mkoani Pemba.

Uajiri katika skuli za Mkoa wa Kaskazini Unguja na Wilaya mbili za Pemba ulipewa upendeleo maalum kutokana na kukabiliwa na ihaba mkubwa wa walimu wa skuli za msingi. Baada ya kutoa ufafanuzi huo naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Mhe. Spika, tunao walimu wengi wa ngazi ya cheti ambao tungeweza kuwaajiri katika skuli za Mkoa wa Mjini Magharibi. Lakni hali halisi katika mkoa huo ni kwamba una walimu wanaozidi mahitaji. Upungufu uliopo katika mkoa huo ni walimu wa masomo ya sayansi, hisabati na kiingereza. Walimu waliozidi katika mkoa huo si wa fani hizo, wangelikuwa walimu waliopo ni wa fani hizo tungeweza kuwapatia ajira. Hivi sasa wizara inaendelea na uajiri wa walimu wenye shahada za ualimu wa skuli za sekondari za wilaya zote za Unguja na Pemba.

(b) Wanayotakiwa kufanya wamiliki wa skuli za binafsi ni kuwaajiri walimu waliosomea katika vyuo vyetu badala ya walimu wa kigeni kwa masomo ambayo walimu wazalendo wanapatikana ambao ndio hao walionbakia katika Mkoa wa Mjini Magharibi na mikoa mingine

ya Unguja na Pemba. Uajiri wa walimu wa kigeni huzingatia masomo ambayo hakuna walimu wazalendo wa kutosha wenye sifa za kufundisha masomo hayo. Wizara inatoa wito kwa walimu wote waliohitimu mafunzo ya cheti cha ualimu ambao hivi sasa hawajaajiriwa, kujiendeleza zaidi ili waweze kupata sifa za juu zaidi za masomo, kwani hivi sasa mahitaji ya walimu wenye vyeti vya ualimu yamepungua sana.

Nam. 47

Tatizo la Ukatwaji wa Minazi Zanzibar

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza :-

Sasa imekuwa ni tabia kwa wananchi kukata minazi kwa kutengenezea mbao na matumizi mengine ya fanicha za nyumbani na mahotelini, huku tabia hii ikitishia janga kubwa la uharibifu wa mazingira na hata kukosekana kwa nazi zenyewe.

Je, wizara imepanga kuchukua hatua zipi kulitokomeza tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 kama hivi ifuatavyo:

Sensa ya miti iliyofanyika mwaka 1997 imeonesha kuwa kuna minazi 5,206,400 Unguja na Pemba. Katika minazi hiyo, karibu nusu ya minazi ilikuwa ni zaidi ya miaka 50 ambayo imeanza kuzeeka na kupungua uzazi. Vile vile minazi mingi imepandwa bila ya kufuata utaalamu unaotakiwa, hali hii imepelekea kutoa mazao kidogo. Aidha, uzazi wa nazi pia umeathirika kutokana na uvunaji wa madafu.

Mhe. Spika, tunakiri kuwa uhifadhi wa rasilimali ya minazi ni jambo muhimu sana, lakini tukubali pia kuwa mnazi ukifikia umri wa miaka 60 hadi 70 unapungua uzazi na unabadilika matumizi yake na hutumika kwa matumizi ya mbao au kuni.

Mhe. Spika, wizara yangu imeandaa utaratibu maalum wa ukataji wa minazi ya aina hiyo, ambapo mhusika anatakiwa kujaza fomu ambayo inapita kwa viongozi wa shehia, wilaya na mkoa ili kutoa maoni yao juu ya minazi iliyoombwa. Idara inayosimamia miti hufanya uchunguzi wa kina na kutoa ruhusa kama minazi iliyoombwa imekubalika kukatwa.

Mhe. Spika, ninasikitika kueleza kuwa kuna minazi mingi inakatwa kwa sababu ya ujenzi wa nyumba za kuishi. Wazanzibari tunatakiwa tubadilishe mfumo wa ujenzi wa nyumba zetu, tutumie maeneo madogo kwa kujenga nyumba za ghorofa.

Mhe. Spika, hatua zinazochukuliwa kulitokomeza tatizo hili ni pamoja na:-

- Kutoa elimu ya kilimo bora cha minazi, umuhimu na uhifadhi wake kupitia Redio, TV na Magazeti;
- Uhamasishaji na uimarishaji wa vitalu kwa wakulima binafsi pamoja na kuzalisha miche ya minazi. Wastani wa miche 200,000 inazalishwa kila mwaka kutoka vitalu vya serikali na vya watu binafsi;
- Uhamasishaji wananchi kuanzisha kamati za uhifadhi katika shehia zao na kutumia sheria ndogo ndogo;
- Kuongeza mashirikiano na Masheha, Wakuu wa Wilaya na Vyombo vya Sheria;
- Kutayarisha sheria ya matumizi ya misumeno ya moto;
- Kufanya utafiti wa mbegu bora ya minazi

Nam. 88

Zanzibar Kuimarisha Bandari Huru

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

Kwa siku nyingi sasa Zanzibar ina azma ya kuwa na Bandari Huru kwa lengo la kukuza biashara huria kati yake na nchi jirani.

(a) Je, serikali ya awamu ya saba imejiandaa vipi kuendelea na azma hiyo.

(b) Je, serikali haioni haja ya kurejesha maeneo ya mabanda ya maonesho kama ilivyo kwa wenzetu wa Tanzania Bara ili kuenda sambamba na azma ya kuimarisha biashara huria nchini.

(c) Kama serikali itarejesha maeneo hayo. Je, yanakusudiwa kujengwa sehemu gani na itahakikisha vipi inayalinda ili yasipotee kama ilivyotokea katika awamu zilizopita.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, katika napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli kwa siku nyingi sasa Zanzibar imekuwa na azma ya kuwa na bandari huru kwa lengo la kukuza biashara huria. Mhe. Spika, katika kuendeleza azma hii nzuri, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba imekuwa ikiharakisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa viwanda pamoja na kuitangaza katika maeneo ya bandari huru na maeneo huru ya kiuchumi (*EPZ*), katika meneo ya Maruhubi, Amani, Fumba na Micheweni.

Hivi sasa serikali ina azma ya kuifanya Zanzibar nzima kuwa eneo tengefu la kiuchumi (*Special Economic Zone –SEZ*) ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kulifanyia kazi hili Mhe. Spika, serikali imekamilisha mchakato wa kumpata Mshauri Mwelekezi atakayepewa kazi ya kufanya utafiti na kuifanya Zanzibar kuwa Eneo Tengefu la Kiuchumi. Utafiti huu unatarajiwa kukamilika Mwezi wa April, 2011.

b) Mhe. Spika haja ya kuwa na eneo la kudumu la Mabanda ya Maonesho ya Zanzibar ipo na nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa, kuweko kwa uwanja wa maonesho Zanzibar itasaidia katika azma ya kuimarisha biashara hapa Zanzibar, pia ni njia moja ya kuitangaza Zanzibar kibiashara na kuiweka katika ramani ya dunia kibiashara.

c) Hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshatenga eneo la hekta 60 liliopo katika maeneo huru ya kiuchumi yaliyoko Dimani katika Wilaya ya Magharibi, kwa ajili ya kujenga Uwanja wa Maenesho ya Biashara (*international Trade Fair*). Hapa Mhe. Spika, nina furaha sana kuwajuilisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba, hatua za awali za kulitengeneza eneo hilo tayari zimeshaanza kuchukuliwa ikiwemo kulipima na kuliwekea uzio, na mchakato wa kuwalipa fidia wananchi wenye vipando vyao katika eneo hilo bado unaendelea.

Aidha, wizara iko katika hatua ya kutengeneza *"Land us plan"* ambayo itaonesha michoro pamoja na gharama za kujenga uwanja huo. Ni matumaini ya wizara kuwa eneo hilo la maonesho litatumika kama ilivyokusudiwa hasa ikizingatiwa kuwa sekta ya biashara ni miongoni mwa maeneo yaliyopewa kipaumbele na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Naomba kuuliza ni nani hasa aliyepewa kazi ya ushauri welekezi.

Pili ni njia gani iliyotumika kumpata mshauri huyo.

Tatu ni kiasi gani cha fedha kilichotengwa kwa utafiti huo wa mshauri mwelekezi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa kuwa masuala haya ya kulifanyia mchakato wa kupima eneo lile bado unaendelea, napenda kumhakikishia kwamba kazi hiyo bado inaendelea kufanyika na hivyo, mshauri mwelekezi bado gharama zinaendelea kutolewa kwa sababu kazi hii inafanywa kwa mashirikiano na Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, yeye ndiye msimamizi mkuu na mlipaji wa mradi huu. Lakini na sisi huwa tunalifuatilia kama ni wizara mama.

Lakini Mhe. Spika, swali lake la pili naomba alirudie kidogo sikulielewa.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, swali langu linasema nataka kujua njia zilizotumika kupatikana kwa mshauri huyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, njia ambayo imetumika ni ile ile ya kutangaza *tender* na baadae kufunguliwa. Baada ya kushauriana na kamati husika kukaa ndipo inapoteuwa mshauri wa kuifanya kazi hiyo na ndio njia iliyotumika Mhe. Spika, lakini gharama zake tutazijua pale kazi itakapokamilika kwa sababu bado mchakato huu unaendelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri amegusia mpango wa muda mrefu wa kutenga maeneo huru, moja ya ahadi ambazo walipewa wananchi wa Fumba na Rais Mstaafu, Dk. Salmin Amour Juma ni kwamba, wangejengewa *Star Seat* katika kipindi chake. Kwa sababu azma hii haikutimizwa wakati ule, sijui lini serikali hii ya awamu ya saba inawaahidi wananchi wa Fumba kwamba wataiona ile *Star Seat* ambayo wameahidiwa miaka mingi iliyopita.

(b) Katika kuendeleza mabanda ya maonyesho vile vile, katika kipindi hicho hicho cha awamu ya tano, serikali ilitumia fedha nyingi sana za walipakodi kujenga eneo la maonyesho katika eneo

la Tunguu ambalo limetumika mara moja tu, na baadae fedha nyingi zile zikapotea kwa sababu halikutumika tena kwa shughuli nyengine. Serikali ina mpango gani wa kuliimarisha lile badala ya kujenga jengine ambalo litatumia fedha nyingi za walipa kodi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba arudie swali, kwa sababu hapa mwisho amekwenda haraka sikulisikia swali nimesikia maelezo tu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, swali la pili nimesema kwamba kwa sababu fedha nyingi za walipa kodi zilitumika kujenga eneo la maonyesho ya kibiashara pale Tunguu ambapo pesa naona kama zimepotea kwa sababu lilitumika mara moja na halijatumika tena. Sasa badala ya serikali kujenga eneo jengine la maoinyesho kama alivyoeleza Mhe. Waziri katika majibu yake. Haoni kama kuna haja ya kuimarisha lile la Tunguu ili kuokoa fedha za walipakodi ambazo zinahitajika sana nchini kwa maeneo mengine.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwanza suala la *Star Seat* na Fumba. Kama anavyojua kwamba ile ilikuwa ni Awamu ya Tano na *strategy* zilizokuwa katika awamu ya tano sasa hivi yashapitwa na wakati na ndio maana tumeajiri mshauri mpya kufanya Zanzibar Eneo Tengefu. Ikiwezekana Zanzibar nzima iwe ni *special economic zone.*

Jambo la pili ni suala la Tunguu. Ni kweli tumetumia fedha nyingi sana kwenye eneo lile na tuliwahi kufanya maonesho mara moja tu. Lakini kwa bahati nzuri palitokea mfandili ambaye alitaka kusaidia mradi wa kujenga Chuo Kikuu cha *SUZA.* Katika masharti yake ilikuwa papatikane eneo ambalo serikali tayari imeshatia *infrastructure* ili kutumia ile infrastructure zile zilizotumika eneo lile pale ilkikuwa ni rahisi kubadilisha moja kwa moja eneo lile likawa ni eneo la Chuo Kikuu cha SUZA Tunguu. Kwa hivyo, pale sasa hivi pana ujenzi na ujenzi huo umeshafika mbali karibu utamalizika na choo karibu kitafunguliwa kwa hivyo, zile *infrastructure* zilizotumiwa hazikupotea bali fedha zimetumika kikamilifu katika kuleta suala muhimu sana la elimu katika nchi yetu, Chguo Kikuu cha *SUZA.* Lakini usiwe na wasi wasi wowote tunafanya kila liwezekanalo kwamba katika hiyo sehemu ya Dimani patajengwa mradi mzuri tu wa maonyesho ya kibiashara na Inshaallah katika kipindi kifupi tu tutaona maendeleo yake. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi naomba kidogo niongezee lile swali la kwanza la nyongeza lililoulizwa na ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa.

Mhe. Spika, katika awamu ya tano mradi wa *Star Seat* haukuwa mradi wa serikali, ilikuwa ni *private company* kutoka India ambao walitaka kujenga mji na wakauita *Star Seat*. Kwa bahati nzuri hawa wenzetu walikuwa wanajenga mji kama huo mkubwa kule Mumbai, India lakini baada ya muda Mhe. Spika, walijikuta wameishiwa na fedha na hatimaye ule mradi ukafa.

Lakini nataka niseme Mhe. Spika, eneo ambalo tumelitenga kule Fumba kwa ajili ya maeneo huru ni eneo ambalo lina zaidi ya hekta 3,000. Hivi sasa tumeanza mazungumzo na kampuni nyengine ambayo tayari tumeshawapa hekta 60 kati ya hizo 3,000 na tayari wameshakuja na michoro kuanza ujenzi wa nyumba na hoteli ambao utaendana na mji tuliokuwa tukiutarajia kama ni *Star Seat*. Wenzetu hawa watajenga katika awamu tatu na hivi karibuni tutapomaliza mazungumzo nao basi awamu ya kwanza ya kujenga nyumba pamoja na hoteli itaanza.

Nam. 78

Uhaba wa Madaktari wa Upasuaji – Pemba

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza :-

Ni muda mrefu sasa Hospitali ya Wete kama zilivyo hospitali nyengine nchini imekosa Wataalamu Bingwa wa magonjwa mbali mbali, kama vile Madaktari wa Upasuaji, ingawa hospitali hiyo ina chumba na vifaa vya kisasa. Jambo hili hupelekea wagonjwa wanaofika hospitalini hapo kwa ajili ya huduma ya upasuaji kulazimika kukimbizwa katika Hospitali ya Chake-Chake au Mkoani. Kitendo hicho huchangia vifo kwa baadhi ya wagonjwa pamoja na upotevu mkubwa wa fedha za umma.

(a) Kwa kuwa gharama za kuwaleta Wataalamu katika Hospitali hiyo ni ndogo mara dufu ukilinganisha na gharama ya mafuta na matengenezo ya magari kwa ajili ya wagonjwa kuelekea Chake-Chake au Mkoani. Je, ni sababu zipi zinazopelekea Serikali kushindwa kuwapeleka wataalamu hawa hospitalini hapo.

(b) Je, Mhe. Waziri utakubaliana nami kuwa Sekta ya Afya Pemba inaleta hisia kama vile Serikali imeamua kuitelekeza kwa kuinyima wataalamu.

(c) Je, Serikali inajua kuwa wataalamu wa Meno kwa Pemba wanaohusika na Hospitali kubwa kama Wete, Mkoani, Chake-Chake n.k. wapo watatu tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Utibabu – Alijibu: -

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 78 lenye vifungu (a), (b) na (c) kjwa pamoja kama hivi ifuatavyo:

(a) Serikali inafanya jitihada kuhakikisha kuwa kuna madaktari katika hospitali zote za Zanzibar ikiwemo ya Wete

Azma ya Serikali ni kuifanya Hospitali ya Wete kuwa ya Mkoa. Ili azma hiyo itimie ni lazima tuwe na Madaktari wa kutosha. Kwa sasa kuna Madaktari bingwa watatu hospitali ya Wete, daktari anayeshughulika na maradi ya wanawake (*Gynaecologist)* ambaye ni mzalendo, *Paediatrician* ambaye ni daktari wa watoto na *Physician* daktari wa maradhi ya jumla kutoka Cuba. Pia yupo daktari mzalendo anayeweza kufanya operesheni za uondoaji wa mtoto wa jicho (*cataract surgeon*).

Jihada zaidi zitachukuliwa kuongeza madaktari katika hospitali hiyo ili kufikia hiyo azma ya kuwa hospitali ya Mkoa.

(b) Mhe. Spika, naomba aondoe hisia kuwa serikali imeamua kuitelekeza sekta ya afya ya Pemba kwa kuwanyima wataalamu. Jambo la msingi ni kuzishughulikia sababu zinazowafanya wataalamu wasipende kufanya kazi huko Pemba au Zanzibar kwa ujumla.

Miongoni mwa hatua za dharura tunazoendelea kuzichukua ni kupunguza makali ya uhaba wa wafanyakazi ni *out-reach programmes* zinazoendelea hivi sasa.

(c) Ni kweli wataalamu wa meno wapo watatu na wanatoa huduma katika Hospital ya Wete, Chake Chake na Vitongoji. Kwa Hospitali ya Micheweni daktari wa meno yupo masomoni Tanzania Bara na huduma hutolewa na daktari kutoka Wete kila Jumanne.

Hospitali ya Mkoani daktari wa meno amestaafu karibuni, utaratibu umeandaliwa kwa madaktari waliopo na wanatoa huduma mara mbili kwa wiki. Wizara inaelewa kuwa hali hii hairidhishi lakini ni ya muda hadi tutapoweza kuwa na wataalamu wa kutosha.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ambayo yameonesha kwamba hospitali ya Wete ina madaktari bingwa ambao wanashughulika na kutoa huduma muhimu sana za kiafya naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa sababu kuna madaktari bingwa ni kwa nini

huduma za upasuaji hazifanyiki pale Wete na badala yake wagonjwa wapelekwe Chake Chake jambo ambalo linachangia kufuja fedha za umma kwa kutumia mafuta na matengenezo ya magari.

Mhe. Spika, swali (b) mawasiliano ni jambo muhimu kati ya mgonjwa na daktari. Katika Hospitali ya Chake Chake Wizara ya Afya imemleta mtaalam kutoka Cuba hajui Kiingereza wala Kiswahili jambo ambalo linaleta usumbufu hata kwa madaktari wengine. Je, hali hii ni nzuri kwa huduma za kiafya.

Mhe. Spika, swali (c) kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba Hospitali ya Wete wanaiandaa kuipandisha daraja na kuwa hospitali ya mkoa. Je, mko tayari sasa kuanzia angalau kwa kujenga chumba cha *mortuary* ili ianze katika huduma hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nimesema kwamba Hospitali ya Wete kuna madaktari watatu, kuna daktari wa wanawake, kuna daktari wa watoto na daktari wa kawaida. Huyo daktari wa upasuaji hayupo kwa hiyo likitokea suala linalohusu upasuaji inabidi mgonjwa apelekwe Chake Chake kwa sababu ndiko aliko daktari. Hilo hakuna jinsi kwa sababu ndiko aliko, kwa hiyo sisi hatupotezi mafuta isipokuwa tunaokoa maisha kumsafirisha mgonjwa kutoka Wete kumpeleka Chake Chake akapate huduma inayohitajika.

Mhe. Spika, jibu (b) daktari kutoka Cuba aliyekuwepo Hospitali ya Chake Chake anajua Kiingereza na ndio maana anafundisha wanafunzi wetu wa Udaktari. Wanafunzi walioko pale wanasomeshwa na madaktari wale na wanasomeshwa kwa Kiingereza. Kwa hiyo, siamini kwamba daktari yule hajui Kiingereza. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Hebu tungepiga makofi kwa utaratibu, akijibu tumepiga makofi tunapoteza muda itabidi yeye hasikiki majibu yake. Nadhani tuwe na utaratibu wa namna ya kupiga makofi katika kupongeza.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, jibu © ili Hospitali ya Wete iwe ya mkoa ina mahitaji mengi ya wafanyakazi, wataalam, vifaa vinavyotakiwa vijalizwe ambapo pale kwenye hospitali havipo. Maandalizi ya hospitali za mikoa sasa hivi yanaandaliwa kwa zile hospitali ambazo zinatakiwa ziwe za mkoa. Tunajaribu kuona kipi kipo, tunaorodhesha wafanyakazi wetu wanaohitajika, tunaorodhesha vifaa vipi vitakavyohitajika, ili tuweze kuona utaratibu wa kuvipata na kuviweka na kuwapeleka madaktari wanaohusika hospitali iweze kufanya kazi.

Kipindi cha miaka mitano hii ndicho tulichojiwekea kufanya hiyo kazi. Kwa hiyo, tutajiandaa na tutajitahidi ili itakapomalizika awamu hii ya miaka mitano hospitali za mikoa ziwe zimeanza kufanya kazi.

Mhe. Spika: Kuhusu mortuary ndio anayouliza lini? Nafikiri tuweke utaratibu wa kwenda kwenye swali linaloulizwa, ukitoa maelezo mengi itakuwa tunapoteza muda na bado swali halikujibika. Mhe. Waziri wa Afya saidia.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu Waziri ni kwamba suala la *mortuary* hata Unguja kuna moja tu Hospitali ya Mnazimmoja tena ndogo wala haitoshi, hospitali nyengine zote hazina. Sasa pale tutakapopata uwezo basi na hospitali ya Wete nayo itajengewa hiyo *mortuary*. Lakini ni suala la upungufu vile vile wa rasilimali.

Kwa hiyo, tunaomba waheshimiwa hilo lifahamike kwamba ni kutokana na upungufu wa rasilimali. Pale tutakapopata nafasi kuiweka hospitali hiyo kuwa ya mkoa bila shaka na *mortuary* tutajenga. Naomba atukubalie hili.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, katika kifungu (b) katika swali la msingi la Mhe. Mwakilishi ameeleza wasi wasi wake jinsi ya wizara inavyoonesha dalili ya kuzitelekeza huduma za afya katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, kwa kuwa wenzetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania *(TPDF)* wameanzisha hospitali nzuri na ya kisasa pale katika kambi ya Ali Khamis *(Ali Khamis Camp).* Kwa hilo napenda nimpongeze Mkuu wa Majeshi pamoja na *CO* wa ile kambi. Kwa kuwa hospitali ile ni ya kisasa na ina vifaa vizuri na yupo daktari mwenye sifa ya *AMO (Assistant Medical Officer).*

Kwa kuwa wanaruhusiwa kupima ukimwi lakini hawaruhusiwi kutoa ushauri nasaha pamoja na kutoa zile dawa za kupunguza makali ya ukimwi. Je, ni lini wataruhusu na pale hospitali ya *Ali Khamis Camp* waweze kutoa dawa pamoja na kutoa ushauri nasaha.

Mhe. Spika, pili kwa kuwa wanaotibiwa pale zaidi ya asilimia 80 ni raia. Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haitoi mgao wa dawa katika hospitali ile. Je, ni lini Wizara ya Afya watatoa mgao wa dawa kwa hospitali ya *Ali Khamis Camp* iliyopo katika Jimbo la Wawi ili watoto wa walipa kodi na wao waweze kunufaika na jasho la wazazi wao.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuna kawaida hii ya kurukia maswali. Swali liliopo ilikuwa linahusu hospitali ya Wete. Sasa kama kuna haja muhimu ya aina hiyo tuwe tunafanya utaratibu wa kuuliza maswali ya msingi.

Vyenginevyo yale maswali yanayoulizwa inakuwa hayapati majibu sahihi kwa sababu tumekwenda kwenye swali la eneo jengine. Haidhuru yote ni ya afya lakini inapanua wigo wa swali kiasi cha kwamba hatimae ile haja ya mjumbe aliyouliza haipatikani. Uliza kwenye swali la msingi.

Nam. 79

Ujenzi wa Vituo vya Afya

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Miongoni mwa sifa kubwa zinazoijengea Zanzibar kwa Sekta ya Afya ni kuvuka malengo ya milenia kwa mueneo wa vituo vya afya katika masafa ya wastani wa kila kilomita 2. Pamoja na mafanikio hayo mazuri ya wizara bado wananchi wetu wamekuwa wakipata tabu sana kufuatilia matibabu kutokana na jiografia ya nchi yetu ilivyo ya visiwa, bahari na miundombinu isiyoridhisha vijijini.

(a) Je, upo mpango wowote kwa kuanzia wa kuanzisha huduma za *outreach services.*

(b) Je, ni lini serikali itaamua kuanzisha madaktari wa vituo vya afya vya mizunguko *(mobile doctors and clinics).*

(c) Kwa kuwa Zanzibar tunao upungufu wa wahudumu wa afya *(PHN+B)* na kwa kuwa baadhi ya wakati huwatumia vijana wanaojitolea *(Red Cross)* kutoa huduma za afya katika maeneo mbali mbali. Je, ni kwa nini sasa kutokana na upungufu wa *PHN* hatutoi mafunzo ya ziada kwa vijana wetu wa *Red Cross* na kuwaajiri ili kusaidia hospitali na vituo vya afya vijijini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 79 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa karibu wananchi wote wa Zanzibar wanapata huduma za afya katika masafa yasiyozidi kilomita 5. Ili kupunguza usumbufu kwa wananchi kufuata huduma wizara imeanzisha huduma za *outreach* kama ifuatavyo:

Madaktari kutoka Hospitali ya Mnazimmoja wanatoa huduma za upasuaji, maradhi ya kinamama, kisukari, maradhi ya viungo na maradhi ya akili katika hospitali za vijijini. Huduma za upasuaji, matibabu ya pua, koo na masikio hutolewa kwa msaada wa *NGO*

ya *Zanzibar Outreach Programme* vijijini Unguja na Pemba kwa mashirikiano ya karibu kabisa na madaktari, wauguzi wa Hospitali ya Mnazimmoja.

Mradi wa Afya ya Kinamama hutoa huduma za afya kwa kinamama na watoto na uzazi wa mpangilio katika Vituo vya Afya kila mwezi kwa utaratibu huu wa *outreach*.

(b) Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na Shirika la Misaada ya Kitabibu kutoka Ufaransa karibuni itaanzisha huduma ya uchunguzi wa *ultra-sound* kwa mzunguko *(mobile ultra-sound services)*. Huduma hizo zitaanza kwa kutolewa katika vituo vifuatavyo: Kivunge, Makunduchi, Kusini, Fuoni, Jambiani na Tumbatu hivi karibuni.

(c) Mhe. Spika, ni kweli wizara inakabiliwa na upungufu mkubwa wa kudumu na inatambua mchango mkubwa na umuhimu unaotolewa na vijana wa *Red Cross*. Ili vijana hawa waweze kuajiriwa itabidi wajiunge na chuo kwa mafunzo rasmi kwa sababu mafunzo wanayoyapata bado hayajawafanya waweze kufanya kazi katika hospitali. Kusaidia ni kitu chengine lakini kufanya kazi kama wafanyakazi wa afya wanahitaji mafunzo maalum. Sasa wanatakiwa vijana hawa wajiunge na chuo kwa mafunzo rasmi kwa kufuata utaratibu ulioko chuoni.

Hata hivyo, wizara iko tayari kuwapatia mafunzo ili kuwaongezea uwezo kila inapohitajika ili kuwaweka katika hali nzuri ya kutoa huduma kwa *up date.* Hili linahitaji kufanyiwa mazungumzo kati ya uongozi wa Wizara na *Red Cross.*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa amesema kwamba wizara yake imejipanga vyema kutoa huduma za *outreach* na *mobile doctors.* Kwa kuwa Zanzibar ni visiwa ndani yake mna visiwa vya Tumbatu, Makoongwe, Kojani, Kisiwapanza na hata Fundo. Je, si vyema huduma hii kwanza ikaanza katika maeneo ya visiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kama ukiangalia hizi huduma zinazotolewa za *outreach* nyingi zinahitaji vifaa na utaalam uliopo pale na usaidizi wa watu walioko katika sehemu ile. Katika sehemu ulizozitaja vituo vilivyoko haviwezi vikakidhi haja ya kuweza kutoa huduma hizo za *outreach* na ndio maana zinafanyika katika zile hospitali kubwa kubwa.

Kwa hiyo, taarifa huwa zinatolewa kwenye matangazo ya redio ili wale ambao wanaokaa sehemu za mbali waweze kutoka kule waliko waende pale wakapate huduma hizo. Vyenginevyo hata kama tutataka ziende kule bila ya kuweza kupata vifaa vile na wafanyakazi wengi wanaotakiwa wakati wa shughuli ile itakuwa haiwezekani. Vituo ulivyovitaja vingi vina mfanyakazi mmoja mmoja ambaye ana shughuli nyengine nyingi kwa hiyo haitawezekana kufanya hivyo. Mhe. Spika, nawaomba Waheshimwia Wawakilishi wote wawasaidie watu wao wanapolisikia tangazo ili waweze kufika katika hivyo vituo vilivyotangazwa wakapate huduma hizo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa swali la msingi linahusiana na vituo vya afya. Kwa kuwa kijiji cha Kibokoni katika Jimbo la Wawi tayari wameshajijengea kituo ya afya na kwa bahati kituo hichi kiliwekwa jiwe la msingi na aliyekuwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk. Ali Moh'd Shein ambaye sasa ni Rais wetu. Kwa kuwa tayari wananchi wameshamalizia kituo kile bado hatua za umaliziaji tu ndogo ndogo ikiwa kama vile plaster pamoja na kupeleka vifaa na kuanzisha kituo hicho.

Je, ni lini serikali itamalizia kituo kile ili wananchi wa Kibokoni waweze kupata karibu huduma ya afya ya mama na mtoto badala ya kuondoka Kibokoni hadi *Vitongoji Cottage Hospital* jambo ambalo linasumbua wajawazito pamoja na watoto.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nilikuwa naomba kwanza niwafahamishe Waheshimiwa Wajumbe kitu kimoja. Sera za Wizara ya Afya ni tofauti na Sera za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambazo mnaambiwa jengeni skuli mkifika *level* fulani wizara itachukua itamalizia.

Mhe. Spika, juzi nilisema kwamba vituo vya afya vimekuwa vingi kiasi ambacho vinakidhi mahitaji. Lakini pale ambapo wananchi watachukua juhudi wakajenga basi Wizara ya Afya kinachowajibika pale ni kuhakikisha kwamba nyinyi mnajenga jengo mnamaliza sisi tunaleta wafanyakazi, sio sisi kumalizia majengo. Lakini hata hivyo, madhali imefikia hivyo hilo tutalitazama na tutaona utaratibu wa kuweza kulimalizia hilo jengo. *(Makofi)*

Nam. 89

Uvutaji wa Huduma ya Umeme kwa Gharama za Wananchi Wenyewe

Mhe. Fatma Mbarouk Said - Aliuliza:-

Ni jambo lililozoeleka kwa wananchi wanaotaka kuvuta umeme kwa mara ya kwanza kulazimika kununua nguzo na waya kwa gharama zao bila ya kurejeshewa fedha zao baadae.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni haja ya Shirika la Umeme kuachana na mpango huo ili kuwapunguzia mzigo wananchi hasa ukizingatia kuwa shirika linaendeshwa kibiashara zaidi kuliko huduma.

(b) Je, nguzo na waya hizi wanazonunua wananchi hao baada ya kuungiwa umeme hubakia ni mali ya nani, ni shirika au wananchi wenyewe.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika (Kny. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati) - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 89 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali hili naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni utaratibu wa mashirika yote ya umeme duniani kugharamia laini inayotoka kwenye *transformer* ya karibu hadi nyumbani kwa mteja ambako hakupaswi kuwa na zaidi ya mita 500. Lakini kutokana na mazingira ya mashirika mengi ya nchi zinazoendelea kama yetu, masafa hayo huweza kufikia hata kilomita moja. Ni gharama ya ziada ambayo bado shirika linaendelea kugharamia. Kuanzia masafa hayo kwenye laini kuu hadi nyumbani kwa mteja huwa ni gharama zinazolipwa na mteja mwenyewe kwa mkupuo mmoja.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa noamba kumjibu swali hilo kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli mara nyingine wateja hugharamia nguzo na vifaa vyengine kwenye njia kuu *(main line)* ya umeme. Hali hii husababishwa na hali ya shirika wakati wa uungaji kwa upande mmoja na haraka ya mteja kuungiwa umeme huo kwa upande mwengine ambapo wateja hujikubalisha kuchangia

gharama hizo. Lakini kiutaratibu ni lazima nguzo na vifaa hivyo viwe mali ya shirika ili liweze kuhudumia laini husika ambayo kwa kawaida huendelezwa kwa wateja wengine. Bila ya hivyo, shirika lingelazimika kupata idhini na ridhaa ya mteja kila mara linapolazimika kufanya matengenezo kwenye njia hiyo kuu ya umeme ambayo inahudumia wateja wengi zaidi ya aliyegharamia. Aidha, bila ya hivyo, gharama hizo kwa mteja zingekuwa endelevu na kwa kuwa angetakiwa kuendelea kuchangia kila mara. Mathalan, shirika lilipolazimika kubadilisha nguzo ama vifaa hivyo.

Mhe. Salum Amour Mtondoo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Bububu Shehia ya Mwanyanya juu Kwagoa walinunua nguzo za umeme kwa ajili ya kupatiwa umeme na tayari wameshapatiwa umeme lakini hivi sasa nguzo hizo zimeoza. Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani wa kubadilisha nguzo hizo ili zisije kusababisha maafa hapo baadae.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika (Kny. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati): Mhe. Spika, tutaangalia hali itakaporuhusu *inshaallah* kulishughulikia suala hilo.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, siku zote serikali huwa karibu na wananchi ambao wamejipanga kwa shughuli za kujiletea maendeleo. Wananchi wa Kijikanigasi, Gasi tayari wamejipanga kwa michango na nguvu zao na kila kitu wamekamilisha kulipa katika Shirika la Umeme na mpaka sasa hivi hawajaunganishiwa umeme huo. Je, ni lini wananchi wa Kijikanigasi watapata huduma hiyo muhimu ya kuunganishiwa umeme.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika (Kny. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati): Mhe. Spika, nchi yetu hii sasa hivi imepiga hatua kubwa katika maendeleo na kila mmoja anahitaji huduma muhimu kama ya umeme. Mhe. Spika, maombi yamekuwa mengi *inshaallah* tutajitahidi kadri itakavyowezekana pale ambapo hali itaruhusu tutaweza kwenda kufanya kazi hiyo.

Nam. 31

Ukosefu wa Umeme kwa Wakaazi wa Shehia ya Tunguu Sokoni

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa wakaazi wa Shehia ya Tunguu Sokoni hawana umeme katika eneo lao. Kwa kuwa maeneo yaliyo karibu na eneo hilo tayari wameshapatiwa umeme.

(a) Ni sababu zipi zinazopelekea serikali kuchelewa kupeleka huduma ya umeme katika eneo hilo huku ikizingatiwa kuwa kipo kituo cha afya ambacho kinahitaji umeme kwa ajili ya huduma za wananchi.

(b) Mhe. Waziri utakubaliana nami kuwa kitendo cha kutowapatia huduma ya umeme wakaazi hao huku wenzao wa karibu wakifaidika na huduma hiyo kinawafanya wawe wanyonge katika nchi yao.

(c) Je, serikali inajipanga vipi katika kukabiliana na changamoto hiyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika (Kny.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati) - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, ni kweli maeneo ya Shehia ya Tunguu Sokoni hayana umeme, hii imetokana na kuwa hayakuingizwa katika mipango ya awamu zilizopita za usambazaji umeme vijijini.

(b) Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ina nia thabiti kuvipatia huduma ya umeme vijiji vyote ambavyo bado huduma hiyo muhimu haijawafikia. Tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kuwa na subira kwani kila hali ya fedha itakaporuhusu vijiji hivyo na vyenginevyo vitasogezewa huduma hiyo.

(c) Serikali itahakikisha kuwa katika mwaka ujao wa fedha kijiji hicho kitaingizwa katika mpango wa kukipatia huduma ya umeme.

Nam. 32

Tatizo la Umeme Mdogo

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa jitihada zake na kuhakikisha kuwa wananchi walio wengi wa Zanzibar wanapata huduma ya umeme mijini na vijijini. Pamoja na jitihada hizo bado kuna baadhi ya maeneo yamekuwa na tatizo la umeme mdogo *(low voltage)* usiokidhi haja ya matumizi yao.

(a) Je, Mhe. Waziri Shirika la Umeme Zanzibar *(ZECO)* tayari limeshafanya tathmini na kujua hali hiyo.

(b) Kama ndio, ni maeneo yepi kwa Unguja yenye matatizo kama hayo.

(c) Je, shirika limejipanga vipi kukabiliana na tatizo hilo na linatarajia kuliondosha ndani ya muda gani

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika (Kny. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati) - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuna baadhi ya maeneo yamekuwa na matatizo ya umeme mdogo na tayari Shirika la Umeme limeshayafanyia tathmini maeneo yote yaliyoripotiwa kuwa na hali hiyo.

(b) Maeneo yaliyoripotiwa na kufanyiwa tathmini kwa upande wa Unguja ni Fuoni, Nyarugusu, Welezo Miembe Saba, Tomondo, Uzi, Mwanyanya, Kwarara, Kisauni, Kihinani, Magogoni, Kiembesamaki, Chukwani, Bwejuu na Jumbi.

(c) Baadhi ya maeneo yaliyotajwa tayari yameshafanyiwa masawazisho, mengine hivi sasa yanaendelea kurekebishwa na Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme. Shirika litahakikisha kuwa matatizo yote yanatatuliwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika kukabiliana na tatizo hili la umeme mdogo shirika limejipanga vipi kuweka *transformer* za akiba na ikiwa

zipo ni ngapi sasa hivi Unguja na Pemba. Kwa sababu ikiwa pahala pamepata wateja wengi *transformer* ile ni ndogo inatakiwa kubadilishwa na kuwekwa kubwa.

Mhe. Spika, swali (b) kutokana na wataalam wanavyotwambia mbali ya kupata *transformer* mafundi huwajibika kufanya utafiti unaoitwa *balancing* kwa zile *phase*. Je, ni utaratibu gani wanaotumia kwa maeneo mengi kama haya kuwa na tatizo hili la umeme mdogo na hali ya kuwa shirika ni shirika la kibiashara.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika (Kny. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati): Mhe. Spika, lazima tuelewe kwamba hivi sasa serikali imefanya juhudi kubwa na inaendelea na juhudi zake. Suala la umeme hasa waya wetu huu umekuwa wa muda mrefu ndio maana serikali imefanya juhudi ya kutaka kubadilisha waya huu. Kwa hiyo, baadhi ya maeneo itaonekana labda kuna matatizo umeme haufiki kutokana na mahitaji ya pale pahala penyewe. Hii inatokana na kwamba wananchi wengi wameunga umeme kwa kutafuta shughuli zozote za kimaendeleo au huduma za nyumbani.

Kwa hiyo, suala la kumjibu kwamba kuna transformer ngapi za *reserve* Unguja na kule Pemba, basi swali hili *inshaallah* tutamjibu kwa maandishi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa kisiwa cha Pemba kimebahatika kupata umeme kutoka Tanga. Je, Mhe. Waziri ni sababu gani ambazo husababisha kukatika mara kwa mara kwa umeme huo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika (Kny. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati): Mhe. Spika, tumelisikia swali lake na tutakwenda kulifanyia kazi *Inshaallah* kwa upande huo huo wa Pemba.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naona muda unakaribia sana kumalizika, tunayo maswali matatu, nadhani tuongeze muda kidogo kama kawaida ili tuyamalize na tupate kuendelea na shughuli nyengine.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja ya kuweka kando muda wa maswali, ili tuweze kukamilisha maswali ya leo yaliyokuwemo kwenye *order paper*. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri Wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Kwa hivyo, tujitahidi leo ni Ijumaa, ili tumalize maswali matatu yaliyobaki kwa kipindi kifupi kidogo, pengine robo saa. Tuendelee na swali linalofuata.

Nam. 92

Uwekaji wa Alama Kwenye Viwanja vya Plan

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak – Aliuliza:-

Kwa kuwa nchi nyingi duniani huweka alama muhimu kwenye viwanja vya plan vinavyotarajiwa kujengwa kama vile njia za kupita na kadhalika, ili kuepusha usumbufu kwa watumiaji wa viwanja hivyo.

(a) Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazopelekea nchi yetu kutokutekeleza suala hili mapema.

(b) Hamuoni kuwa kuendelea na mfumo huu tulionao tunawasababishia usumbufu wananchi wetu kwa kuwa endapo utaiziba njia iliyozoeleka kupitwa unalazimika kuwatengenezea njia mbadala watumiaji wa njia hiyo kwa wakati ule.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: (Kny: Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati) - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 92 lenye vifungu (a), na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba nchi nyingi duniani huweka alama muhimu za upimaji (*beacons*) katika maeneo yanayotengwa kwa ajili ya njia ya huduma nyengine za kijamii wakati wa upimaji wa viwanja, ili kuepusha usumbufu kwa watumiaji wakati wa uendelezaji wake.

Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba suala hilo la uwekaji wa alama katika maeneo ya njia na huduma nyenginezo, pia linatekelezwa katika nchi yetu wakati wa upimaji wa viwanja.

Mhe. Spika, tatizo liliopo ni kwa baadhi ya alama hizo hung'olewa wakati wa uendelezaji na usafishaji wa njia katika maeneo hayo. Aidha, kwa bahati mbaya au kwa makusudi. wizara yangu kupitia Idara yake ya Upimaji na Mipango

Miji huwa inachukua hatua muwafaka ya kuzirejesha alama hizo kila inapopata taarifa.

Mhe. Spika, kimsingi jukumu la wizara yangu kupitia Idara yake ya Upimaji na Mipango Miji na Utayarishaji wa ramani za maeneo husika pamoja na upimaji wake, upimaji ambao unajumuisha uwekaji wa alama za upimaji za kila huduma. Kazi za uwekaji wa alama nyengine kwa mfano alama za njia, za mitaa n.k. zinapaswa kufanywa na taasisi husika na kazi hizo.

Nam. 81

Utunzaji wa Historia ya Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Kila nchi duniani inayo historia yake na hivyo ndivyo ilivyo Zanzibar. Lakini Wazanzibari wa leo (Vijana) na wale watakaokuja siku za usoni huenda wakashindwa kuijua historia ya nchi yao kwani wataalamu mbali mbali wamekuwa wakieleza kuwa historia ya Zanzibar imevamiwa kwa maksudi na inapotoshwa kwa kuandikwa visivyo.

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipo haja ya kutafuta wataalamu (wanahistoria) na kupewa kazi maalum ya kuandika ilivyo sahihi Historia ya Zanzibar.
(b) Kama wapo watu wanaopotosha historia hiyo kwa makusudi au vitabu vilivyoandika vibaya historia ya Zanzibar, Serikali inapanga kuchukua hatua gani.
(c) Ni eneo lipi kati ya Zanzibar na Bagamoyo lililokuwa kitovu cha biashara ya utumwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwanza nakiri kuwa ni kweli Historia ya Zanzibar imepotoshwa na baadhi ya waandishi wakiwemo wataalamu wanaoandika Historia ya Zanzibar, ili kukidhi maslahi yao binafsi kwa mnasaba huo, nakubaliana na ushauri wa Mhe. Mwakilishi kuwa ipo haja ya kutayarishwa Wataalamu, wenye uwezo na kupewa jukumu la kuandika Historia sahihi ya Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, hatua za awali za kuandika vitabu na vijarida zimeanza kuchukuliwa, pamoja na kuwapeleka wafanyakazi wetu masomoni katika vyuo mbali mbali. Kwa wale wanaopotosha historia kwa makusudi, wizara italifuatilia suala hili kwa lengo la kurekebisha kasoro hiyo. Aidha, wizara yangu kupitia Chuo cha Utalii hutoa mafunzo maalumu kwa vijana wanaopitia katika Chuo hicho kuhusiana na Historia na Utamaduni wa Zanzibar.

(c) Mhe. Spika, Soko Kuu na Kitovu cha Biashara ya Utumwa ilikuwa Zanzibar, Bagamoyo ilikuwa ni sehemu ya kupitia (*Transit Point*). Kabla ya kusafirishwa kupelekwa Zanzibar ambako kulikuwa na Soko Kuu. Kutoka Zanzibar, watumwa walikuwa wakisafirishwa kupelekwa nchi mbali mbali, zikiwemo visiwa vya Bahari ya Hindi kama Mauritius, Seychelles, Re-Union, Arabuni na wengine walibaki Zanzibar kufanya kazi za kilimo cha mikarafuu na minazi na wengine wakitumika kwa kazi za majumbani.

Nam. 82

Ongezeko la Watalii Baada ya Maridhiano Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Baada ya Wazanzibari kufikia maridhiano hapo tarehe 5 Novemba 2009 na kuanza kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar, kasi ya uongezeko la watalii Zanzibar imekuwa kwa mujibu wa taarifa za taasisi husika.

(a) Je, Mhe. Waziri kabla ya Maridhiano Zanzibar ilipokea watalii wangapi na wameongezeka wangapi kwa mwaka.

(b) Kuongezeka kwa watalii tegemeo ni kuongezeka kwa mapato. Je, tangu kupita kwa Mardhiano Sekta ya Utalii imechangia kiasi gani katika pato la Taifa.

(c) Kwa kuwa dunia imefurahi sana na hatua ya Wazanzibari ya kufikia Maridhiano. Je, kwa hatua hiyo Zanzibar itafaidika vipi na suala la "*package tourism*".

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mwaka 2008 Zanzibar ilipokea watalii 128,440 idadi iliongezeka kufikia 135,954 mwaka 2009 sawa na asilimia 6 na 2010 idadi hiyo ilishuka kidogo hadi 132,836 kutokana na matatizo ya mabadiliko ya hali ya hewa.

(b) Utalii umekuwa ukichangia asilimia 25 katika pato la taifa na asilimia 70 ya makusanyo ya fedha za kigeni. Hata hivyo, ni muda mfupi tokea kipindi cha maridhiano kuweza kutambua kama kuna mabadiliko ya uchangiaji katika pato la Taifa yanayotokana na maridhiano hayo. Kwa uzoefu watalii wote huandaa safari mapema, kwa hiyo matokeo ya mabadiliko ya nchi au mazingira ya kituo huonekana aghalabu mwaka unaofuata.

(c) Zanzibar inafanya utalii wa aina zote za utalii (package tourism and independent) na kukua na kuendelea kuwa utalii hutegemea sana hali ya usalama na utulivu wa nchi. Kwa kuwa kuna maridhiano hayo tunategemea utalii wetu kuimarika zaidi. Hata hivyo, Zanzibar kwa sasa haiwezi kujiondoa katika aina hii ya utalii (*package*) kutokana na ukweli kwamba:

- Ni fikio la mbali kwa masoko yetu (*long haul destination*)
- Hatuna mashirika yetu ya ndege ambayo yatasaidia kuleta watalii wa kujitegemea (*independent travelers*)
- Kukosa wageni wengi wanaojireejea (*repeat tourists*)
- Utalii wa Vikundi (*Package tourism*) ni mtizamo/mfumo wa uendeshaji Utalii ulimwenguni ambapo watalii wengi huhofia usalama wao wakati wa kusafiri katika soko geni.

Licha ya malalamiko mengi kuwa aina hii ya utalii huwa haifaidishi nchi husika kwa vile pesa hulipwa nje. (*Package Tours*) una faida zifuatazo kwa Zanzibar.

- Kuongeza pato la wazalendo kwa kufanya matembezi (*excursions*)
- Kuongeza pato la fedha za kigeni kutokana na kodi wanazolipa Kodi ya VAT, VISA ada za viwanja vya ndege ada ya vingilio katika maeneo ya Utalii.
- Vile vile kuisaidia kutangaza soko la Zanzibar katika masoko ya nje na kuiweka katika ramani ya ulimwengu.

- Utalii huu hulinda soko la Zanzibar wakati wa misukosuko. Mfano wakati wa mtikisiko wa uchumi duniani.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba anielimishe. Kwa kuwa amekiri kwamba faida moja ya *Package Tours* tunayoipata ni malipo yanayotokana na VISA. Ninavyojua mimi VISA hulipwa kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Je, Zanzibar tunafaidika vipi na suala hili la VISA.

Mhe. Waziri Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, mapato kutokana na suala la VISA ni kweli huwa wanalipa katika Ubalozi wa Tanzania, lakini vile vile kuna kasma ambayo huwa inakuja moja kwa moja katika Serikali ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, naomba niongezee majibu juu ya swali lililoulizwa na Mhe. Hija Hassan kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kuna taratibu mbili ambazo zinatumika kwa ajili ya kulipia VISA.

Kwanza mtalii anaweza akalipa VISA nchini anakotoka, yaani nchini kwake ambapo zinakwenda Ubalozi wa Tanzania. Fedha hizo kwa mujibu wa utaratibu Balozi za Tanzania zinatumia fedha hizo kulingana na makubaliano ya kasma zao zilizopitishwa ndani ya bajeti.

Lakini vile vile watalii wanaweza wakaja moja kwa moja wakapata VISA katika uwanja wa ndege wa Zanzibar, kwa Kiingereza wanaita *VISA on Arriver*. Fedha ambazo tunazikusanya hapa Zanzibar, fedha zile ni fedha za Muungano. Lakini kwa makubaliano ya mwaka 1996 yaliyofanywa na Mhe. Waziri wa Fedha wa Zanzibar wakati ule alikuwa Mhe. Amina Salum Ali na Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati ule alikuwa Professor Mbilinyi, ni kwamba mapato yote ya Muungano yanayokusanywa Zanzibar yatabakia na yatatumiwa Zanzibar.

Kwa maana hiyo Mhe. Spika, alivyosema Mhe. Waziri ni sahihi, kwamba fedha za VISA zinazopatikana moja kwa moja hapa Zanzibar, tunazikusanya na kuzitumia sisi Zanzibar.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa fedha zinazostahiki kuwekwa katika mikono ya hazina ya Zanzibar, ni zile ambazo

yule mtalii anakuja hapa moja kwa moja. Je, hizi fedha ambazo mtalii anakuja Zanzibar, lakini kalipia kule kule kwenye nchi anayotoka, kuna utaratibu gani wa fedha zile kuletwa Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo: Mhe. Spika, tuna makubaliano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba kila mwaka kuna fedha zinazotoka katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuingia katika bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa maana ya kwamba yale makusanyo yaliyokusanywa kwa njia moja wapo kama hii ambayo aliyoiuliza Mhe. Mwakilishi, basi na sisi huwa tunapata gawio la asilimia 4.5. Kwa hivyo, fedha hizo pamoja na fedha nyengine huwa kila mwaka tunapata na sisi gawio.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, tunavyofahamu kwamba watalii wanaokuja wana madaraja mbali mbali. Kuna watalii wa daraja la kwanza na kuna watalii vishuka.

Je, Mhe. Spika, hawa watalii wa daraja la kwanza na hawa watalii vishuka, wanalipa sawa sawa VISA zao?

Mhe. Waziri Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, naomba arudie tena swali lake, sijasikia vizuri.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, nauliza kwamba hawa watalii wanaokuja nchini wanakuja wa daraja mbali mbali. Kuna wa daraja la kwanza na kuna wa daraja la chini kabisa, tunawaita vishuka. Je, katika kulipa hizo VISA zao, watalii vishuka na wa daraja la kwanza wanalingana malipo yao katika VISA?

Mhe. Waziri Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, watalii hao kwa kweli hawalingani wanatofauti.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo: Mhe. Spika, inawezekana Mhe. Waziri hakumsikia au hakumfahamu vizuri Mhe. Mwakilishi swali lake.

Mhe. Spika, nataka nijibu swali la Mhe. Ali Abdalla Ali kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kabla ya kutokea msuko suko wa kiuchumi wa dunia, nchi yetu ilikuwa ina VISA tofauti kulingana na nchi sio kulingana na aina ya mtalii, kwa mana ya kwamba baadhi ya nchi zilipaswa kulipia VISA Tanzania ya dola 100, baadhi ya nchi zilipaswa kulipia VISA Tanzania dola 50 na kuna baadhi ya nchi zilipaswa kulipia VISA Tanzania hata dola 20.

Mhe. Spika, lakini baada ya hapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilijikuta kwamba watalii wengi hawaji Tanzania kwa sababu ya ule msuko suko wa kiuchumi uliotokea, ambao ulimkumba mtalii moja kwa moja. Tukatafuta mkakati wa kuweza kupata watalii. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia bajeti yake ya mwaka 2008/2009 ikafanya maamuzi ya kupunguza VISA na kuziweka VISA zote ziwe ni dola 50.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo mtalii akiwa kishuka, akiwa daraja la kwanza au akiwa daraja la pili VISA zao wote ni sawa sawa, kwa sababu yale ni malipo ya kuingilia nchini, sio malipo ya mtalii wa aina gani anapaswa kuingia nchini. Mtalii mwenyewe kulingana na hali yake, ndiye anayechagua akae katika hoteli gani kulingana na hali yake. Lakini VISA zote ni sawa sawa hazitegemei na aina ya mtalii.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuanza uchaguzi wa Naibu Spika, nimepata ombi la Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa tuna shughuli maalum ya uchaguzi katika Baraza lako tukufu na kwa kuwa wajumbe wako wanahitaji kushauriana katika kamati za chama ili tupate uwamuzi mzuri wa kupata viongozi wetu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba tuliahirishe Baraza lako kwa muda wa saa moja, mpaka saa 5:30 asubuhi hii ili tuweze kurudi katika Baraza hili. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja hii haijadiliwi ni ya kuuliza tu moja kwa moja. Wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nafikiri labda tungezingatia jambo moja, sina hakika kwamba tutakuja kuwahi maana leo ni siku ya Ijumaa. Nadhani tuahirishe moja kwa moja mpaka jioni, ili tupate ule muda mzuri wa kushughulikia jambo hili. Ninavyoelewa jambo lenyewe ni kuhusiana na uchaguzi huu huu, ili kuufanya uchaguzi uende vizuri na bora zaidi.

Sasa tusirudi saa 5:30, muda utakuwa ni mfupi na hatutoweza kumaliza. Kwa kuwa tunaahirisha moja kwa moja mpaka jioni, kabla ya kuahirisha naomba nichukuwe nafasi hii nina maombi kidogo hapa niyatangaze, ili tuweze kuendelea na shughuli yetu.

Kwanza nina ombi la Wizara ya Afya. Inasemekana katika nchi jirani kumetokea janga la maradhi. Ni vizuri nchi majirani basi tuwe tunapeana taarifa linapotokea janga la aina hiyo. Sasa nadhani itakuwa sio taarifa ya muda mrefu. Nataka nimuombe Mhe. Naibu Waziri wa Afya atowe taarifa hiyo ili tuipate na tujuwe kama kuna maelekezo ya wizara yake namna ya kujipanga tuelewe. Mhe. Naibu Waziri wa Afya, karibu utowe taarifa hiyo.

TAARIFA

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nitowe taarifa mbele yenu, kuhusu maradhi ambayo yameingia katika nchi jirani ya ugonjwa wa machano, wengine wanaita homa ya manjano.

Mhe. Spika, ningependa kwanza nitowe maelezo kidogo kuhusu hoja ya machano

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, ielekee *microphone* ili sauti itoke vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Hewallah bwana *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Spika, najua tumezowea kuona mtu labda ana macho rangi ya machano, homa za manjano ziko nyingi na zina sababu tofauti. Lakini tunayotaka kuyazungumza hapa leo sio yale ya kawaida tuliyokuwa tumeyazowea. Kwa mfano mtu amepata malaria anapata machano labda anatatizo la ini hapana.

Mhe. Spika, huu ugonjwa wa machano tunaouzungumzia leo ni maradhi ambayo sasa hivi yamejitokeza nchini Uganda na ni maradhi ambayo yanasababishwa na mbu. Mhe. Spika, ni virus ambao wanaenezwa na mbu kutoka kwa mgonjwa mmoja kwenda kwa mgonjwa mwengine.

Mhe. Spika, mpaka dakika hii hapa Zanzibar maradhi hayajaingia, isipokuwa mbu wanaosababisha maradhi hayo wapo. Watu wanakwenda na kurudi kutoka nchi nyengine kuja huku, kwa hivyo huwenda hili tatizo likajitokeza. Kwa hivyo, tumepewa taarifa tutowe tahadhari.

Mhe. Spika, ugonjwa huu hauenezwi kwa watu kugusana. Maana tena tusije tukawanyanyapaa wenye ugonjwa wa homa ya manjano, hapana. Mbu ndio tatizo liliopo. Kwa hivyo, kama mbu tunao tunaweza tukaupata huu ugonjwa

wakati wowote, isipokuwa tu tahadhari tunayotakiwa tuifanye ni tuhakikishe usafi katika maeneo yetu ili mazalia ya mbu yasitokee ili tuweze kujikinga na wale mbu waliopo.

Mhe. Spika, ugonjwa huu umeingia Uganda watu 256 wameambukizwa na kati ya hao watu 50 wamekufa, kwa sababu ni *virus* haina matibabu, kama tunafahamu *virus* hakuna matibabu. Kipindi kipite, aidha u-*recover* au uwende, moja katika mawili hayo.

Mhe. Spika, hapa kwetu hatujawahi kupata mgonjwa yeyote. Tahadhari tunayoichukuwa, tumetoa taarifa katika vyombo vya habari, tumewaandikia kila taasisi zilizopo hapa Zanzibari, ili kuchukua tahadhari na kuwataka wasafiri wachanje, kwa sababu kuna chanjo ya maradhi haya.

Kwa hivyo, katika bandari zote wageni wataulizwa vyeti vya chanjo watakapoingia, ili kuona kwamba kila anayeingia anachanjwa. Kwa hivyo, tutakuwa tuko salama kwa upande wa wageni wanaoingia.

Vile vile tunawaombeni Waheshimiwa Wajumbe, wale ambao wanasafiri basi wahakikishe nao wanachanja, ili kujitengenezea kinga na dawa ziko wizarani kwenye sehemu ya chanjo.

Pia tahadhari nyengine tuliyochukua, watalii wote wametakiwa wakija waoneshe vyeti hivyo kutoka kwao. Kwa sababu taarifa imetolewa kwa Idara ya Mambo ya Nje kutoa taarifa katika Balozi zetu za nje ya nchi. Kwa hivyo, kilichobaki kwetu sisi sasa, kama jukumu letu ni kuhakikisha kwamba mazalia ya mbu hayapo, tunapotoka nje tuchanje, hiyo ndio kinga peke yake tuliyonayo. Kwa hivyo, hiyo Mhe. Spika, ndio taarifa fupi niliyotaka kuiwasilisha kwenu. Ahsante Mhe. Spika *(Makofi).*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri hajatupa dalili za maradhi hayo, kwamba ukiona una dalili hii basi ujuwe ndio tayari umeupata. Mhe. Spika, tungeomba tupate na dalili za maradhi hayo.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, hebu hapo hapo ulipo, kama unaweza ukatusaidia dalili za maradhi, ili wajumbe waweze kupeleka ujumbe mzuri kwa wananchi wao, kwamba mwananchi akijihisi yuko namna hii au namna hii basi afanyeje na akimbilie kwa haraka gani hospitali. Labda ungetupa taarifa zaidi Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali kuhusu haya maradhi. Mhe. Spika, hivi sasa hapa kwetu kuna maradhi mengi tu ambayo yanasababisha manjano, itakuwa kwanza sio rahisi

mtu kujitambua kwamba hili ndio hili au ndio lile. Kwa hivyo, ukiona kwanza manjano tu yoyote ile inatokeza mwilini mwako basi kimbilia hospitali.

Lakini Mhe. Spika, huu ni ugonjwa ambao unasababishwa na mbu, unaanza kupata homa kama mafua, unajisia kama mtu mchovu vile, kama vile mtu anayeugua mafua, viungo vinauma, utapata homa za vipindi. Lakini baadae kwa ghafla unaanza kuona macho yamegeuka ya manjano na mwili unakuwa wa manjano, ambapo ni tofauti na manjano nyengine zinavyoanza.

Kwa hvyo, ukiona vitu kama hivyo yaani uchovu wa mwili, homa ndogo ndogo na mwili unaanza kugeuka wa manjano naomba tukimbilie hospitali. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Tunashukuru Mhe. Naibu Waziri, kwa taarifa yako hiyo. Nafikiri Waheshimiwa Wajumbe mtaipokea hiyo taarifa na tutakuwa tunajihadhari kama alivyotuelekeza Mhe. Naibu Waziri, yeye akiwa ni daktari.

Waheshimiwa Wajumbe, labda nataka niongezee jambo moja tu kwamba Mhe. Waziri wa Afya aliniomba jambo hili alitowe haraka Mhe. Naibu Waziri kwa sababu ya hali halisi ya namna ya kuenea kwake na jinsi ambavyo limeathiri kule nchini Uganda. Kwa hivyo, hawakuwahi kutayarisha ile taarifa rasmi kama kauli ya serikali, lakini kwa tahadhari waliona kwamba litufike mapema jambo hili. Kwa sababu leo tunamaliza shughuli hizi basi tusingekuwa na muda mwingine wa kutoa taarifa hii, isipokuwa kipindi hiki. Kwa hivyo, niliona ni busara kwamba tumpe nafasi hiyo ili atowe taarifa hiyo.

Nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari wakutane katika chumba nambari 2 cha kamati, kwa ajili ya kufanya kazi yao ndogo iliyobaki ya kuhesabu kura, walikwishafanya uchaguzi wao, kwa hivyo ilibaki kazi ya kuhesabu kura, kwa hivyo waende kuifanya kazi hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe, matangazo mengine ambayo nimeobwa, hii ni kwa ajili ya kuwajua viongozi wetu tu, lakini ni uchaguzi unaohusu Jumuiya ya UWAWAZA, ambayo tulitangazia itafanya uchaguzi nafikiri ilikuwa sijui ni jana au juzi. Sasa wameniomba kwa kuwa viongozi hawa ni kati ya wajumbe wetu, basi tuwajuwe viongozi wetu waliochaguliwa ni nani na nani. Kwa hivyo, nimeombwa kwamba nitangaze matokeo kwa wajumbe, ili Waheshimiwa Wajumbe wapate faida ya kuwajua nani viongozi wa Jumuiya hiyo ya UWAWAZA.

Waheshimiwa Wajumbe, bahati mbaya maelezo hayako vizuri sikujua kama kulikuwa na wagombea wangapi. Lakini uchaguzi umefanyika ambapo kura

zote zilizopigwa ilikuwa 17, kura zilizoharibika ni 3 na kura zilizokataa hakuna, kura zilizomchagua mgombea ni 14 na mgombea mwenyewe alikuwa ni Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Kwa hivyo, nimeombwa nitangaze kwamba Mhe. Mgeni Hassan Juma, ndio Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo ya UWAWAZA.

Waheshimiwa Wajumbe, Mwenyekiti huyu ana msaidizi wake yaani Makamu Mwenyekiti. Kura zilizopigwa zilikuwa ndio hizo hizo 17, kura zilizoharibika ni 5, kura ambazo zilikataa hakuna, kura ambazo zilimchagua mgombea wa nafasi hiyo Mhe. Ashura Sharif Ali ni 12. Kwa hivyo, naomba nitangaze rasmi kwamba Mhe. Ashura Sharif Ali amechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo ya UWAWAZA. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe, nafasi ya Mtunza Hazina. Kura zilizopigwa ni 17, kura zilizoharibika hakuna, kura zilizokataa hakuna, kura zilizomkubali Mhe. Salma Mussa Bilal ni 13, kura zilizomkubali Mhe. Sira Ubwa Mamboya ni 2. Kwa hivyo, nimeombwa nitangaze kwamba Mhe. Salma Mussa Bilal amechaguliwa kuwa Mtunza Hazina. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe, kulikuwa na nafasi nyengine 4 za Ujumbe wa Kamati Tendaji. Kura zilizopigwa ni 17, zilizoharibika hakuna, kura zilizokataa hakuna, kura zilizomkubali Mhe. Asha Abdu Haji ni 8, kura zilizomkubali Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej ni 9, kura zilizomkubali Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa 9, kura zilizomkubali Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi ni 9, kura zilizomkubali Mhe. Viwe Khamis Abdalla ni 4, kura zilizomkubali Mhe. Shadya Mohammed Suleiman ni 12, kura zilizomkubali Mhe. Panya Ali Abdalla ni 6, kura zilizomkubali Mhe. Asha Bakar Makame ni 7. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe wanne wafuatao wamechaguliwa kuwa Wajumbe wa Kamati Tendaji ya Umoja wa Wawakilishi Wanawake Zanzibar yaani UWAWAZA.

Waheshimiwa Wajumbe wenyewe ni Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, ambaye alipata kura 12, Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej kura 9, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na yeye amepata kura 9 na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na yeye amepata kura 9.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe hao ndio waliochaguliwa katika Jumuiya hiyo na ndio viongozi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe, kuhusu mikutano hii ya *caucas.* Nimeombwa nitangaze kwamba mkutano wa *caucas* ya wajumbe kutoka chama cha CUF, watakutana ukumbi wa juu pale mara baada ya kuahirisha kikao hiki hivi punde.

Kwa upande wa *caucas* ya wajumbe wa CCM wao wameniomba watumie ukumbi huu, na mimi nimekubali, hivyo watakutana katika ukumbi huu mara baada ya kuahirisha kikao hiki.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni, wakati ambao tutashughulika na masuala ya uchaguzi na hatimaye kumuomba Mhe. Balozi kutufungia mkutano wetu huu, ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe *(Makofi).*

(Saa 5:03 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, karibuni tena katika kikao chetu cha jioni hii, kwa ajili ya kuendelea na shughuli zetu. Lakini kabla hatujaendelea mafundi wangu wamenipa taarifa kwamba mitambo inaleta tabu kidogo kiasi kwamba mawasiliano yanaweza kuwa sio mazuri.

Pamoja na hivyo, napokea taarifa hivi sasa ambayo ni *breaking news* kwamba sasa mawasiliano ni mazuri humu ndani. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, Katibu tuendelee na utaratibu.

UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama tulivyoachia pale kipindi cha asubuhi kazi ya jioni hii tunaazia na masuala ya uchaguzi. Kwa hivyo, moja kwa moja tuanze na Uchaguzi wa Naibu Spika na matayarisho yote ameniambia Mkurugenzi wa Uchaguzi kwamba yako tayari nadhani nimpe nafasi atoe maelezo kwa nafasi hizo mbali mbali za Naibu Spika, Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Tume. Mkurugenzi wa Uchaguzi Katibu wa Baraza.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, ahsante kuhusu Uchaguzi wa Naibu Spika. Kifungu cha 74 cha Katiba kinaelekeza kwamba Naibu Spika atachaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, pia Kanuni zinaelekeza kwamba kila Chama cha Siasa chenye Uwakilishi ndani ya Baraza kinaweza kuleta jina la Mgombea wa Kiti cha Naibu Spika.

Kwa hivyo, nimepokea majina mawili kutoka Vyama vya Siasa kwa ajili ya kugombea nafasi hiyo, jina la kwanza ni Mhe. Ali Abdalla Ali kutoka Chama cha Mapinduzi akiwa ni Mgombea wa Kiti cha Naibu Spika na jina la pili ni Mhe. Rashid Seif Suleiman kutoka Chama cha Wananchi CUF akiwa ni Mgombea wa Kiti cha Naibu Spika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Katiba inaelekeza kwamba kama ulivyo utaratibu wa Uchaguzi wa Spika pia Uchaguzi na Naibu Spika utakuwa kwa Kura ya Siri.

Nadhani sasa ni vyema kwa heshima na atadhima tugawe karatasi za kura, ili Waheshimiwa Wajumbe muweze kupiga kura ya kumchagua Naibu Spika.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, nakushukuru kuhusu utaratibu, ingekuwa ni vyema tukahesabiwa na kwa ajili ya kuelewa *quorum* na halafu ndio zikagaiwa *ballot papers*. *(Makofi)*

Katibu wa Baraza: Waheshimiwa Wajumbe, idadi ya Wajumbe ambao wamo ndani ya ukumbi kwa hivi sasa ni 59.

TAARIFA

Mhe. Amina Iddi Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana. Utaratibu tunatakiwa mabosi tutakayotilia kura tuoneshwe kama hayana kura.

Katibu wa Baraza: Wahudumu bado kugawa karatasi ya kura, tumekupeni muwenazo ili muweze kuwa standby na bado kupiga kura, kwa sababu pia tumerekebisha Kanuni zetu za Baraza, kwamba Wagombea watapewa nafasi ya kujieleza kila mmoja na baadaye kuulizwa maswali yasiyozidi matatu na hapo ndipo tutakapopiga kura. Kwa hivyo, wahudumu bakieni na karatasi mpaka nitakapokwambie kugawa kura pamoja na masanduku yote yaletwe mbele.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naona kuna wajumbe wengine wanaingia.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, wajumbe watatu wameingia na kufanya idadi ya wajumbe kuwa 62.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumekubalina kwamba itakapofika wakati wa kutaka kupiga kura kwa nafasi hizi zilivyo ni Spika, lakini tayari yeye ameshatoka. Sasa kwa upande wa Naibu Spika, nadhani wapate nafasi ya

kujieleza. Kwa mujibu wa karatasi niliyonayo kuna wagombea wawili ambao ni Mhe. Ali Abdalla Ali na Mhe. Rashid Seif Suleiman.

Kwa hivyo, nitangulie kumkaribisha Mhe. Ali Abdalla Ali, ili atoe maelezo kwa muda usiozidi dakika tatu. Katibu wa Baraza, kuna maelekezo yoyote ya Kanuni kuhusu muda wa kujieleza.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, Kanuni inasema atatoa maelezo na kuomba kura. Kwa hivyo, maelezo atakayoona yanafaa ya kuweza kuwashawishi wajumbe wamchague.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tutumie dakika tatu kwa ajili ya maelezo na hatimaye kama kuna maswali matatu, basi tunaweza kuruhusu yaulizwe. Sasa nimuombe Mhe. Ali Abdalla Ali apande hapa juu, ili atoe maelezo yake.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kutoa maelezo yangu binafsi kwa nafasi niliyoomba. Mimi naitwa Ali Abdalla Ali ni Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini kuanzia mwaka 1995 hadi leo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, uwezo ninao, uzoefu nimepata kwa muda mrefu, nia pamoja na sababu ninazo. Waheshimiwa Wajumbe pande zote mbili naomba kura zenu. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kuna swali.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii kuweza kumuuliza swali moja Mhe. Ali Abdalla Ali ambaye ni Mgombea wa nafasi ya Naibu Spika. Kwa kipindi kirefu tulikuwa hatuna mtu ambaye ni mtetezi katika Baraza hili.

Je, Mhe. Mjumbe unagombea nafasi hii utatusaidia nini sisi Wawakilishi wa wananchi katika majimbo yetu ndani ya Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwa kweli swali la Mhe. Mjumbe ni zuri, nadhani peke yangu siwezi kuamua kila kitu, isipokuwa tutashirikiana sote kwa pamoja na tutafanya utaratibu kwa kufuata Kanuni, sheria pamoja na Katibu na baadaye tuweze kutoa maamuzi ambayo yatafaa kwa sote. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, swali jengine. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe tunakuruhusu rudi kwenye nafasi yako.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana naomba kura za wajumbe wote pamoja na yako. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimkaribishe mgombea mwengine ambaye ni Mhe. Rashid Seif Suleiman. *(Makofi)*

Mhe. Mjumbe karibu sana unazo dakika tatu za kujieleza na kama maswali yapo Waheshimiwa Wajumbe watakuuliza.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kutoa maelezo yafuatayo. Mimi kwa jina naitwa Rashid Seif Suleiman, *profession* yangu ni mwalimu nilipata *Degree* ya mwanzo Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam ya Sayansi na Ualimu mwaka 1980. baadaye nikasoma *Advance Diploma* ya *Educational Administration* katika Chuo Kikuu cha Leds.

Vile vile nimewahi kuwa Mwalimu Mkuu Mkaguzi wa Sekondari katika skuli za Pemba na hiki ni kipindi changu cha pili katika Baraza la Wawakilishi kupitia Jimbo la Ziwani. Kwa kuwa uwezo ninao kama mnavyoniona katika michango yangu na utetezi, basi naomba mnichague kama Naibu Spika, kwa sababu nyengine moja kubwa Mhe. Spika, alikuwa mbele yangu kwa darasa moja. Kwa hivyo, mkinipa mimi Naibu Spika nafikiri mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kuna maswali, naam nimemuona Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante anataka kumuuliza Mhe. Mgombea kwamba hivi sasa yeye yuko *backbenchers*, kwa kuwa *backbenchers* mara nyingi hatuna watetezi. Je, akipata nafasi atatutetea. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe arejee swali lake sijalisikia vizuri.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rejea swali. Katibu wa Baraza zima *microphone* yako kidogo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, nasema hivi Mhe. Mgombea ametokea katika nafasi ya *backbenchers* katika Baraza hili na hivi sasa unataka nafasi ya kuwa Naibu Spika utakuwa sehemu ya mbele. Je, utakapopata hii nafasi utawatetea *backbenchers*, kwa sababu hivi sasa hawana watetezi. *(Makofi).*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kweli swali zuri na linakwenda moja kwa moja mimi nitaanza kumtetea Mhe. Spika mpaka *backbenchers*, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na Mhe. Mgombea ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati yangu naomba kumuuliza swali. Mhe. Mgombea katika Baraza hili kuna akinamama ambao mara nyingi sana viti vyao vinakuwa kidogo. Je, Mhe. Mjumbe ukipewa nafasi hii utawatetea vipi akinamama ili viti vyao viwe vingi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hapana hili si swali la Naibu Spika na hilo ni suala la kisiasa kwa upande mmoja na pia ni mambo ya Kikatiba. Kwa hivyo, swali hilo hatuliruhusu.

Swali la mwisho Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mgombea swali moja tu, Baraza letu ni Mjumbe wa *Commanwealth Parlimentary Association (CPA)* na wewe Mhe. Spika ni shahidi kwamba umekuwa ukihudhuria vikao hivyo ambavyo vyengine Lugha ya Kiswahili hakizungumzwi.

Je, inapotokea wewe Mhe. Spika hukwenda vikao hivyo na ukamtuma anayekusaidia na huyu ambaye atapata nafasi ya Naibu Spika. Hivi Mhe. Mgombea unao uwezo gani wa kuliwakilisha Baraza hili mikutano ya Kimataifa ambapo Lugha ya Kiswahili haizungumzwi. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kweli swali ni zuri ambalo ameuliza Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Kwa hivyo, naomba nilihakikishie Baraza hili kwamba mimi uwezo ninao wa kwenda katika mikutano ya Kimataifa hasa ya *CPA*, kwani Mhe. Spika mwenyewe niliwahi kumwakilisha katika mkutano mmoja kule Mozambique. Kwa hivyo, ninamshukuru na alijua kuwa ninao uwezo wa kumwakilisha. Vile vile baada ya kurudi nilimletea ripoti pamoja na makabrasha yote yaliyotolewa kule, ili Baraza liweze kufaidika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, maswali yamekwisha na Mhe. Mjumbe rejea kwenye nafasi yako.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wanipe kura zao zote, ili niweze kuendelea na huduma muhimu ya Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Katibu wa Baraza, kabla ya kugawa kura nafikiri kuna Waheshimiwa Wajumbe wengine wameingia. Kwa hivyo, si vibaya tukapata idadi ya Waheshimiwa Wajumbe wote.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Waheshimiwa Wajumbe ambao wamo ndani ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi hivi sasa ni 66. Kwa hivyo, *box* la kura hili hapa na tunalifunga kwa utaratibu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kura hii ni ya siri na wala hatukutengeneza *Ballot House*, lakini kwa heshima yenu Waheshimiwa Wajumbe, naamini kila mmoja ataificha kura yake isikopiwe na mtu mwengine.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, sasa tugawe karatasi za kura kwa Waheshimiwa Wajumbe, wahudumu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa ni wakati wa kugawa karatasi za kura. Maswali hakuna. Haya Mhe. Mgeni Hassan Juma chukua nafasi yako. *(Makofi)*

UCHAGUZI WA MWENYEKITI KWA NAFASI YA MWANAMME

Katibu wa Baraza: Waheshimiwa Wajumbe, tunaanza zoezi la upigaji kura, wa nafasi ya Mwenyekiti, wanaume.

Mhe. Spika: Kampeni basi tena, Mhe. Mjumbe rudi huko nyuma. *(Kicheko)*

Mhe. Spika: Waheshimwia wajumbe, yuko mjumbe ambae hajapata karatasi ya kupigia kura hakuna sasa tupige kura. Kwenye kundi la wanaume unachagua mmoja na kundi la wanawake unapiga kura ya ndio au hapana.

Nadhani nyote mshapiga kura, kwa hivyo tukusanye kura.

TAARIFA

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hiyo karatasi ya kura ya ndio au hapana hatujapewa bado, tumepewa ya wanaume lakini ya ndio au hapana ya wanawake hatujapewa.

Mhe. Spika: Iliyogaiwa sasa hivi ni hiyo tu, sasa tukusanye kura ya kundi la wanaume. Wakati tunakusanya kura hizo kwanza tusubiri ya Mhe. Mgeni ili tuweze kuomba mawakala kama mnahitaji.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, tunagawa moja moja, sasa hivi tutapiga ya wanaume tukimaliza kukusanya tutapiga nyengine.

Mhe. Spika: Kumbe ni hiyo tu iliyogaiwa kwa hivi sasa. Sasa tukusanye kura za kundi la wanaume. Walati tunakusanya kura hizo nafikiri tusubiri na ya Mhe. Mgeni Hassan Juma ili tuweze kuomba mawakala kama mnahitaji.

Waheshimiwa wajumbe, sasa nafikri nyote mmeshatumbukiza kura ndani ya sanduku nashukuru.

Katibu wa Baraza: Sasa tunagawa karatasi za kura kwa ajili ya mwenyekiti Mwanamke na ni mgombea mmoja kwa hivyo tunapiga kura ya ndio au hapana.

Mhe. Spika: Nafikiri Waheshimiwa wajumbe wote mmepata karatasi ya kura sasa pigeni kura na tayari katibu ameonyesha sanduku kwamba hamna kitu, tupige kura.

Nategemea tayari mmeshapiga kura kwa hivyo naomba tukusanye kura. Hapa waheshimiwa wagombeya walitakiwa kutoa mawakala wao katika kuhesabu kura zao.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa taarifa katika uchaguzi huu kuna mjumbe mmoja aliongezeka kwa hivyo idadi ya kura zilizopigwa ni 68 wakati ule uchaguzi wa mwanzo idadi ya kura zilizopigwa zilikuwa ni 67.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, mimi namteua Mhe. Salehe Nassor Juma kuwa wakala wangu. Inaonekana amekubali.

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, mimi namteua Mhe. Salim Awadh Salmin awe wakala wangu. Inaonekana amekubali.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, mimi namteua Mhe. Viwe Khamis Abdalla kuwa wakala wangu. Inaonekana amekubali.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe nafikiri kura zote zimeshakusanywa.

UCHAGUZI WA WAJUMBE WATATU WA TUME YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI

Katibu wa Baraza: Kanuni zinaelekeza kwamba Baraza lichague wajumbe watatu kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wajumbe ambao si Mawaziri, si Manaibu Mawaziri wala sio Mwanasheria Mkuu

kugombea nafasi hizo. Kutokana na marekebisho ya kanuni tuliyofanya tulisema kwamba nafasi hizi sasa zitagawiwa kwa mujibu wa uwiano wa vyama, kwa mujibu wa uwiano wa uwakilishi uliokuwapo katika Baraza maana yake ni kwamba upande wa Chama cha Mapinduzi utapata nafasi mbili, na upande wa Chama cha Wananchi CUF utapata kiti kimoja.

Lakini kanuni inaelekeza kwamba jinsia izingatiwe kwa hivyo katika nafasi hizi upande wa Chama cha Mapinduzi ambao wao walikuwa na nafasi mbili, nafasi moja imetengwa kwa ajili ya wanawake. Na upande wa CUF wao walikuwa na uhuru wa kuweza kuleta *candidate* kama ni mwanamke au mwanamme, kwa hivyo majina tuliyoyapokea katika nafasi hizi ni kama ifuatavyo na tutapiga katika makundi matatu.

Kundi la kwanza ni uchaguzi wa Mjumbe wa Tume ya Baraza la Wawakilishi kwa wagombea wanawake CCM, kanuni pia inaelekeza kwamba kila chama cha siasa kinaweza kuleta jina moja au majina yasiyozidi matatu kwa kila nafasi. Chama cha Mapinduzi katika nafasi za wanawake kimeleta majina mawili.

1.	Mhe. Asha	Bakari	Makame
2.	Mhe. Raya	Suleiman	Hamad

Katika kundi hili Baraza linatakiwa kuchagua mmoja kati ya hawa wawili.

Kundi la pili litakuwa ni uchaguzi wa Mjumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi CCM wanaume, Chama cha Mapinduzi kimeleta jina moja ambae ni Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando *(Makofi)*

Kwa kundi hili Baraza litatakiwa lipige kura ya kumkubali au kumkataa mjumbe huyu.

Kundi la tatu la nafasi za uchaguzi ni uchaguzi wa Mjumbe wa Tume ya Bajeti ya Tume ya Baraza la Wawakilshi kutoka Chama cha Wananchi CUF, chama cha CUF kimeleta jina la Mhe. Hija Hassan Hija. *(Makofi)*

Ambapo Baraza litatakiwa kupiga kura ya kumkukubali au kumkataa mgombea huyo, kwa hivyo Mhe. Spika, naomba uwaite waheshimiwa wagombea ili waweze kujieleza.

TAARIFA

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Nafasi za wanawake kwa vile ni nafasi moja niliyogombea mimi na mama Asha Bakari Makame mimi nafasi naondoa. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Raya Suleiman Hamad yeye anaomba kuondoa jina lake kanuni zinasemaje Katibu.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, kanuni zinaruhusu mgombea kuondoa jina lake kwa hivyo litabakia jina moja ambalo tutalipigia kura ya kumkubali au kumkataa.

PENDEKEZO

Mhe. Omar Ali Shehe: Kwa kuwa kila nafasi ina mgombea mmoja mmoja mimi nadhani kwa Baraza hili tukubaliane kwamba hawa ndio waliopita.

Mhe. Spika: Vipi katibu tutakuwa tumetekeleza kanuni tukifanya hivyo, maana imeelekezwa kwamba akiwepo mmoja tunapiga kura ya ndio au hapana au tunatenga kanuni kando. *(Kicheko)*

Basi kama tunatenga kanuni kando mmoja atoe hoja sasa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Kutokana na sababu hiyo basi naomba nipendekeze mbele ya kiti chako kwamba kwa hoja hii tukubali kuweka kanuni kando.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubali hoja ya mjumbe wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kukubaliwa)

Mhe. Spika: Kwa hivyo tutawatangaza hawa kwamba wamechaguliwa rasmi.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, kutokana namaamuzi hayo zoezi la chaguzi hizi tatu limekamilika kilichobakia ni kwamba tunaomba utupe muda wa nusu saa kwenda kuhesabu kura za Naibu Spika, na wenyeviti wawili.

Mhe. Spika: Sasa Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri tuwape muda wenzetu wakahisabu kura na Katibu watendaji weko ni nani wanaohesabu kura.

Katibu wa Baraza: Katika katika sisi Makatibu wawili tuliokuwepo hapa kuna na timu ya makatibu wengine watatu wakiongozwa na Shehe Saleh Ali Salim Afisa Mdhamini Baraza la Wawakilishi Pemba ndio tutakaoshiriki katika zoezi hili la kuhesabu kura. Pamoja na mawakala waliochaguliwa na wagombea wenyewe.

Mhe. Spika: Nafikiri tunakubali hilo, kwa hivyo baada ya shughuli hiyo nafikiri tuwape muda secretariat wende wakahisabu kura na kwa maana hiyo itabidi tuahirishe kwa muda mfupi ili baadae tuje kutoa matangazo na hatimae tumalize shughuli iliyobakia.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala: Mhe. Spika, nilikuwa nadhani kwamba tupendekeze ikiwezekana wakati zoezi la kuhesabu kura linafanyika kama kanuni zinaturuhusu, tumwachie Makamo wa Pili wa Rais afanye shughuli iliyobakia.

Mhe. Spika: Ikibidi hivyo inabidi Makatibu hawa wasiondoke na Mkurugenzi wetu wa uchaguzi ateue timu kwa niaba yake ili waje kufanya shughuli hiyo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nafikiri utaratibu huo hauwezekani kwa sababu Makamo wa Pili wa Rais anatakiwa kuhitimisha kazi ya shughuli zetu, kwa hivyo kuhirimisha ni baada ya uchaguzi na matokeo, pengine hata hawezi kusema chochote kuhusu matokeo. Kwa hivyo haiwezekani hiyo.

Mhe. Spika: Nafikiri tukubaliane tukahesabu kura kiasi nusu saa, kwa hivyo tuahirishe kikao hiki mpaka baada ya nusu saa na turudi saa 12.30.

(Saa 12.00 jioni Baraza liliahirishwa mpaka saa 12:40 jioni)

(Saa 12:40 Baraza lilirudia)

MATOKEO YA UCHAGUZI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru watendaji wetu kazi ya kuhesabu kura imemalizika, matokeo yako tayari. Nimejaribu kuangalia matokeo haya wale walioteuliwa kuwa mawakala wote wametia saini kuthibitisha kwamba kazi ya kuhesabu kura imekwenda vizuri na haikuwa na matatizo yoyote. Kwa hivyo, naomba sasa nichukue nafasi hii kutoa matokeo ya uchaguzi tulioufanya punde kwa nafasi zote ambazo tumezifanyia uchaguzi hivi punde.

Matokeo ya Uchaguzi wa Naibu Spika

Yafuatayo ni matokeo ya uchaguzi wa Naibu Spika, uliofanyika leo Ijumaa tarehe 28/01/2011. Kama mtakavyokumbuka kwamba katika

nafasi hii ya Naibu Spika, iligombewa na Waheshimiwa wawili wakiwa ni Mhe. Ali Abdalla Ali pamoja na Mhe. Rashid Seif Suleiman. Matokeo ni kama ifuatavyo.

Idadi ya wapiga kura wote zilizopigwa katika uchaguzi huu wa Naibu Spika, ilikuwa ni kura 67, kura zilizoharibika hakuna. Kura alizopata Mhe. Rashid Seif Suleiman ni kura 28, idadi ya kura alizopata Mhe. Ali Abdalla Ali ni kura 39. Kutokana na matokeo hayo namtangaza rasmi Mhe. Ali Abdalla Ali amechaguliwa kuwa Naibu Spika, wa Baraza hili la Nane la Wawakilishi Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2010/2015. (*Makofi*).

Naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza rasmi Mhe. Ali Abdalla Ali kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika.

Matokeo ya Uchaguzi wa Wenyeviti

Katika uchaguzi huu tuliofanya pia tuliwachagua wenye viti wa Baraza. Katika kundi la wanaume tutakumbuka kwamba waliogombea nafasi hiyo ya uwenyekiti ilikuwa ni Mhe. Abdalla Juma Abdalla pamoja na Mhe. Mahmoud Moh'd Mussa . Matokeo ya kura ni kama ifuatavyo. Idadi ya kura zilizopigwa katika uchaguzi huo wa Mwenyekiti itakumbukwa kwamba alizidi mjumbe mmoja ilikuwa ni kura 68. Kura zilizoharibika hakuna, udadi ya kura alizopata Mhe. Abdalla Juma Abdalla ni 32. Idadi ya kura alizopata Mhe. Mahmoud Moh'd Mussa 36. Kutokana na matokeo hayo Waheshimiwa Wajumbe naomba kuchukua nafasi hii kumtangaza rasmi Mhe. Mahmoud Moh'd Mussa kuwa amechaguwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza hili la Nane la Wawakilishi la Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2010/2015. (*Makofi*).

Tumefanya kazi ya kumchagua Mwenyekiti, mwengine na kama mtakumbuka kwamba kanuni zinaelekeza kuzingatia jinsia. Kwa hiyo nafasi hii ya kundi la wanawake iligombewa na Mhe. Mgeni Hassan Juma ambaye idadi ya kura zilizopigwa katika uchaguzi huo ni 68, kura zilizoharibika ni 3, idadi ya kura zilizomkataa Mhe. Mgeni Hassan Juma ni 12, na idadi ya kura zilizomkubali Mhe. Mgeni Hassan Juma ni 53.

Kutokana na matokeo hayo Waheshimiwa Wajumbe namtangaza rasmi Mhe. Mgeni Hassan Juma kuwa amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2010 /2015. (*Makofi*)

Nampongeza sana Mhe. Mgeni kwa kuchaguliwa.

Matokeo ya Uchaguzi wa Wajumbe wa Tume ya Bajeti

Wajumbe watatu ambao watakuwa ni wajumbe wa Tume ya Bajeti. Tutakumbuka kwamba Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Raya Suleiman Hamad kwenye kundi la wanawake yeye alijitoa na kwa hiyo katika uchaguzi huo wajumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza wakawa wamebakia wagombea mmoja mmoja kwa makundi yote, kundi la wanawake, kundi la wanaume CCM na kundi la wanaume CUF. Kutokana na hoja ambayo ilitolewa na tukaikubali waheshimiwa wajumbe, wajumbe wafuatao wamechaguliwa rasmi kuwa wajumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, nao ni:

1) Mhe. Asha Bakari Makame,
2) Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)
3) Mhe. Hija Hassan Hija.

Waheshimiwa Wajumbe nachukua nafasi hii kuwapongeza wote hao kuwa Wajumbe wa Tume ya Bajeti.

Uteuzi wa Mnadhimu Mkuu

Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka kwamba katika marekebisho yetu ya Kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi yalifanyika katika mkutano huu. Tulikubaliana kwamba kutakuwa na Mnadhimu Mkuu wa Serikali huwa anateuliwa na Serikali. Naomba nitoe taarifa rasmi kwenu kwamba Serikali imemteuwa Mhe. Moh'd Aboud Moh'd (Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais) kuwa Mnadhimu Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ataitumikia nafasi hiyo akimsaidia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kufuatana na kifungu cha Kanuni kifungu cha Nam. 14 cha Kanuni zetu mpya za Baraza la Wawakilishi.

Matokeo ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Club ya Baraza la Wawakilishi

Waheshimiwa Wajumbe tutakumbuka juzi na jana nilitangaza kwamba kutakuwa na uchaguzi wa Club yetu ya Michezo. Naomba nitoe taarifa kwamba uchaguzi huo ulifanyika na nimeombwa na Club hiyo ambayo mlezi wake ndio mimi, nitoe taarifa ya matokeo ya uchaguzi huo na wale waliochaguliwa kwa nafasi mbali mbali.

Mwenyekiti wa Club yetu ya Michezo ya Baraza la Wawakilishi. Aliyegombea nafasi hiyo alikuwa ni Mhe. Hamza Hassan Juma. Na kwa hivyo Mhe. Hamza

Hassan Juma amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Club ya Michezo ya Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha mwaka 2011/2015. (*Makofi*)

Matokeo ya Makamo Mwenyekiti wa Club

Halkadhalika walifanya uchaguzi wa Makamo Mwenyekiti wa Club hiyo. Aliyegombea alikua ni Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando). Naomba nichukue nafasi hii kutoa taarifa kwenu kwamba Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) amechaguliwa kuwa Makamo Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi.

Matokeo ya Katibu wa Club

Club hiyo vile vile imemchagua Katibu nafasi ambayo iligombewa na Mhe. Haji Omar Kheir.

Naomba nichukue nafasi hii kutoa taarifa kwamba Mhe. Haji Omar Kheir amechaguliwa kuwa Katibu wa Club ya Michezo ya Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha 2011/2015.

Matokeo ya Katibu Msaidizi wa Club

Msaidizi Katibu nafasi ambayo iligombewa na Mhe. Ali Salum Haji. Naomba nitoe taarifa kwamba Mhe. Ali Salum Haji amechaguliwa kuwa Msaidizi Katibu wa Club ya michezo ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2011/2015.

Matokeo ya Meneja wa Time

Meneja wa timu kwa kawaida anakuwa ni mtu mzito sana. Nafasi hiyo imegombewa na Mhe. Omar Yussuf Mzee. Kwa hiyo naomba nitoe taarifa rasmi kwamba Mhe. Omar Yussuf Mzee amechaguliwa kuwa meneja wa timu ya Club ya Baraza la Wawakilishi kipindi cha 2011/2015.

Matokeo ya Meneja Msaidizi

Idadi ya wajumbe waliogombea nafasi ni watatu (3) ambao walikuwa ni Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Wanu Hafidh Ameir. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, Mhe. Nassor Salum Ali na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Kura walizopata katika uchaguzi huo Mhe. Mohammed Mbwana Hamad lipata kura 7, Mhe. Nassor Salum Ali alipata kura 35, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk 2. Kwa hivyo naomba kutoa taarifa rasmi kwamba Mhe. Nassor Salum Ali amechaguliwa kuwa Meneja Msaidizi wa timu ya Club ya Michezo ya Baraza kwa mwaka 2011/2015.

Matokeo ya Uchaguzi wa Wajumbe Wanne wa Halmashauri ya Club

Idadi ya Wajumbe waliogombea ni 8 ambao ni kama ifuatavyo:

	Wagombea	**Idadi ya Kura**
1)	Mhe. Asha Abdu Haji	32
2)	Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	54
3)	Mhe. Shadiya Mohammed Suleiman	40
4)	Mhe. Asha Bakari Makame	31
5)	Mhe. Aviwe Khamis Abdalla	31
6)	Mhe. Farida Amour Mohammed	11
7)	Mhe. Sira Ubwa Mamboya	40
8)	Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.	19

Kwa hivyo naomba nichukue nafasi hii kuwatangaza wajumbe 4 wa Halmashauri waliochaguliwa kuwa ni:

1) Mhe. Asha Abdu Haji
2) Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji
3) Mhe. Shadiya Mohammed Suleiman
4) Mhe. Sira Ubwa Mamboya

Wote hawa wamechaguliwa kuwa wajumbe wa Club ya Michezo ya Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha mwaka 2011/2015.

Waheshimiwa Wajumbe hiyo ndio taarifa ya chaguzi mbali mbali ambazo tumefanya leo na nyengine zimefanyika jana. Naomba kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa matokeo hayo. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimkaribishe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi. (*Makofi*).

HOTUBA YA MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR, MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI KATIKA UFUNGAJI WA MKUTANO WA PILI WA BARAZA LA WAWAKILISHI, TAREHE 28 JANUARI 2011

Mhe. Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenye wingi wa rehema kwa kutuwezesha kutekeleza kwa ufanisi mambo yote tuliyoyapanga katika mkutano wetu huu wa pili kwa salama na amani na kutekeleza wajibu wetu katika Baraza lako tukufu.

Nakushukuru wewe Mhe. Spika kwa kuendesha mkutano huu kwa mafanikio makubwa.

Halikadhalika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kwa kuuliza maswali mazuri kuhusu utendaji wa shughuli za Serikali na kutoa maoni yao wakati wa kujadili miswada na hoja mbali mbali zilizowasilishwa hapa Barazani. Vile vile, napenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri kwa kuyajibu vizuri na kwa ufasaha maswali yaliyoulizwa pamoja na kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali. Ni matumaini yangu kwamba wananchi wamefaidika na majibu hayo.

Mhe. Spika, katika mkutano huu jumla ya maswali ya msingi 90 yaliulizwa na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri pamoja na maswali mengi ya nyongeza. Pia Baraza lilijadili hoja mbili, taarifa mbili na kufanya semina mbili kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Halikadhalika Baraza lilipitisha Miswada miwili ya Sheria ambayo ni kama ifuatayo:-

1. Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uendelezaji, Ukuzaji na Uwekaji wa Viwango Bora wa Bidhaa na Usimamizi wa Huduma Zinazolingana na hizo na
2. Mswada wa Sheria ya Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, Mswada wa kwanza kujadiliwa katika Baraza lako Tukufu ulikuwa na lengo la kuimarisha huduma za biashara kwa pande zote mbili, mnunuzi na muuzaji na kuimarisha hadhi ya nchi yetu kibiashara. Kama tunavyofahamu kuwa kwa muda mrefu Zanzibar ilikuwa ikijulikana kuwa kitovu cha biashara kwa Kanda ya Afrika Mashariki kabla na baada ya Mapinduzi. Jambo hili lilipelekea wafanyabiashara na watu wa mataifa kadhaa kuja kutembelea na kufanya bishara zao hapa Zanzibar. Hali hiyo ndio iliopelekea hivi leo kuwa na makabila mchanganyiko yenye kupendeza na haiba katika jamii yetu.

Katika siku za hivi karibuni hali hii ilibadilika na nchi yetu kukaribia kuwa jaa la makachara kwa bidhaa zisizokuwa na viwango vinayohitajika na pia watu wetu kuhatarishiwa maisha kwa kuingizwa nafaka na bidhaa zilizopitwa na muda wa matumizi. Hii ni hatari tena kubwa sana sio kwa afya ya wateja na walaji pekee bali hata katika suala zima la kuimarisha uchumi wetu. Matokeo yake hadhi ya ufanyaji biashara imepotea na hivi sasa tunalazimika kuchukuwa juhudi kubwa

ili kuweza kuirudisha hadhi hiyo jambo ambalo linahitaji muda na gharama kubwa.

Mhe. Spika, kwa mfano, moja ya mitaji yetu mikuu ni utalii, huduma bora, uwaminifu na biashara, kwa maana hiyo suala la kuwa na viwango vya biashara vinavyokubalika lina umuhimu mkubwa kwetu.

Mhe. Spika, napenda kusisitiza kwa kusema kuwa Zanzibar bila ya biashara haijakamilika, hata kihistoria umaarufu wa Visiwa vya Zanzibar umetokana na biashara. Hivyo ndiyo kusema kuwa biashara ndio mhimili muhimu wa kuinua fursa za ajira hapa Zanzibar na ndio sehemu kubwa ya mapato na nguvu za kiuchumi kwa watu wa Zanzibar na itaendelea kuwa hivyo kwa muda mrefu ujao. Kutokana na hali hiyo, Serikali lazima iendelee kuchukua jukumu la kusimamia kazi ya uendelezaji, ukuzaji na uwekaji wa viwango na ubora wa bidhaa zinazoingia au kutoka nchini.

Nimepata faraja kuona kuwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wametumia fursa hii kuujadili kwa kina mswada huu.

Madhumuni ya sheria hii, Mhe. Spika, ni kukuza shughuli za uwekezaji nchini pamoja na kudhibiti viwango na ubora wa bidhaa zinazoingizwa na zile zinazozalishwa nchini. Kwa mujibu wa mswada huu hapana shaka kazi ya Taasisi husika itaweza kufanyika kwa ufanisi zaidi, ikitiliwa maanani kuwa juhudi za kuimarisha ubora wa viwango vya bidhaa mbali mbali kwa ajili ya biashara ni suala muhimu.

Mhe. Spika, ni muhimu kuainisha kuwa chini ya mswada huu, Serikali itakuwa na mamlaka ya kuunda vyombo au Taasisi za kisheria zitakazotumiwa kuhakikisha kuwa wafanyakazi wa Taasisi hizo wanawajibika katika kudhibiti ubora wa bidhaa, ukaguzi wake pamoja na kuimarisha mashirikiano na wadau wengine ndani na nje ya nchi.

Aidha, sheria hii itaweka mazingira mazuri katika mfumo wa ushindani wa kibiashara na kushajiisha uzalishaji wa bidhaa za ndani na kuiwezesha sekta binafsi kwenda sambamba na kufuata masharti ya viwango vya kimataifa kwa kuzingatia mpango wa kitaifa wa usafirishaji bidhaa nje ya nchi.

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, wenyewe ni mashahidi wa kuwepo kwa mtindo hivi sasa kwa baadhi ya wafanyabiashara ndogo ndogo kuuza bidhaa zilizopitwa na wakati

kwa punguzo kubwa la bei ili kuwavutia wateja ambao pasi na kujuwa kuwa wanahatarisha maisha yao na familia zao.

Mhe. Spika, maeneo kama vile Darajani na Soko kuu la Zanzibar kumeshamiri kuwepo kwa biashara ya bidhaa hizo zilizopitwa na wakati kama vile juisi za mapaketi, tungule za vibati, mafuta ya kupikia, samli na hata vipodozi. Tabia hii sio nzuri inaweza kuhatarisha afya za wananchi wetu. Wananchi hawana budi kuwa waangalifu wa bidhaa za aina hii.

Mhe. Spika**,** Mswada wa pili kujadiliwa katika Baraza hili tukufu ulikuwa mswada wa Sheria ya kuweka miundo, uendeshaji na usimamizi wa utumishi wa umma, ambao mtakubaliana nami kuwa mswada huu nao ni mzito sana kwa vile unagusa moja kwa moja masuala ya maslahi ya rasilimali watu katika jamii yetu.

Rasilimali watu ndio yenye mchango mkubwa katika njia za kuinua au kuangusha uchumi wa nchi, kwa sababu hata ikiwa kutakuwepo na nyenzo bora za mapato, kama hakuna watendaji bora na makini wa kuyasimamia vyema katika ukusanyaji na utunzaji wake, Serikali haitafaidika nayo.

Aidha, utendaji kazi katika uzalishaji ukiwa hafifu tija haitopatikana. Kwa mnasaba huo suala la utumishi wa umma na nidhamu kazini linahitaji mazingatio makubwa sana. Kwa hivyo, mswada huu umekuja katika wakati muafaka na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa kuupa mswada huu uzito unaostahili.

Mhe. Spika, ni jambo lililowazi kabisa kuwa kutokana na sababu mbali mbali za kiutumishi yakiwemo maslahi ya wafanyakazi, utendaji wetu Serikalini umeshuka na hivyo kupunguza ufanisi na tija kwa kiasi fulani.

Hili halihitaji mwenge wa kulimurika liko wazi kwa sababu baadhi ya athari zake zinaonekana. Mathalan tumekuwa tukiambiwa hatuna wataalamu wa kutosha katika fani mbali mbali, lakini Serikali inachukuwa juhudi kila siku kusomesha watu wake, hata hivyo kutokana na mazingira magumu ya utumishi tuliyokuwa nayo wengi kati yao hukosa uzalendo na kukimbilia nchi jirani jambo ambalo huzidisha matatizo kwetu.

Mambo haya hatutaki yaendelee kutokea ndio maana ya kuupitisha mswada huu kwa kauli moja. Kwa kufanya hivyo, jamii imeona malengo yetu na naamini tutafanikiwa. Kama Wachina wasemavyo, **"safari ya maili elfu moja huanza na hatua moja"** sisi tumeanza naomba tuwe na subira ili tufikie malengo yetu. Natoa wito kwa wafanyakazi wote Serikalini kuona juhudi zetu hizo na kuziunga mkono kwa kutimiza wajibu wao ili hayo tuliyakusudia yafanikiwe.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kuwa mkutano wetu huu ulitanguliwa na hoja mbili, hoja ya kwanza ilikuwa inahusu marekebisho ya kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Hoja hii imekuja kufuatia mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar yaliofanywa mwaka jana yaliowezesha kuwa na muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Nashukuru kuwa marekebisho hayo yamefanyika vizuri na yametupa uwezo wa kuendesha vikao vyetu kwa ufanisi bila ya matatizo. Ni matumaini yangu kwamba kila Mjumbe atazipitia kwa makini kanuni hizi.

Mhe. Spika, hoja ya pili ilikuwa kujadili Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein aliyoitoa tarehe 11 Novemba, 2010 wakati alipolizindua Rasmi Baraza hili la Nane la Wawakilishi la Zanzibar. Katika kujadili hoja hiyo, tumejionea wenyewe umuhimu wa hotuba hiyo ambayo sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumeiona kuwa ni dira ya kutuonyesha njia ya tunakotaka kwenda. Kwa hapa sina la kuliongeza zaidi ya kutoa shukrani kwa Wajumbe wote waliochangia, kwa michango yao mizuri ambayo imewapa wananchi wetu matumaini makubwa juu ya Serikali yao.

Mhe. Spika, ni jambo la kawaida kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kujifunza kwa njia za Semina kabla ya kujadili baadhi ya miswada na mambo yanayohitaji kuwasilishwa hapa Barazani. Hivyo, Ndugu Wajumbe safari hii walipata fursa ya kuelimishana kwa njia ya Semina Mswada wa Sheria unaohusiana na mambo ya Utumishi wa Umma na semina ya pili ambayo inategemewa kufanyika Jumapili tarehe 30 Januari, 2011 itakayoelezea masuala ya Maendeleo ya Mawasiliano ya Simu Zanzibar kupitia Kampuni ya *ZANTEL*. Napenda kuishukuru sana Kampuni ya *ZANTEL* kwa kututayarishia semina hiyo ambayo itatuelimisha kwa kina mambo wayafanyayo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya naomba uniruhusu nieleze suala muhimu la kuhusu biashara ndogo ndogo Darajani (Dada Njoo). Serikali ilikuwa ikipata malalamiko kutoka kwa wananchi kutokana na

usumbufu na bughudha wanazopata wanafunzi wa Skuli za Darajani na Vikokotoni. Kwa kuepuka malalamiko hayo Serikali imetenga eneo la Saateni na kutengenezwa eneo maalum kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo ndogo ili kuwapa utulivu wanafunzi wetu. Ndiyo maana Serikali kupitia Baraza la Mji wa Zanzibar imewataka wafanyabiashara hao kuondoka katika eneo hilo.

Natumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Mkurugenzi wa Baraza la Mji wa Zanzibar kwa kuchukua hatua madhubuti katika kulisimamia suala la kuwarejesha wafanyabiashara hao Saateni kutoka eneo hilo la Darajani ili kuwapa nafasi ya kutosha na kuwawezesha vijana wetu kupata elimu kwa utulivu. Aidha, nalishauri Baraza la Mji la Zanzibar kuliendeleza eneo hilo ili liwe zuri, safi na lenye mazingira bora.

Kwa sababu ya kutaka kulitunza vizuri eneo hilo, Serikali kupitia Baraza lako Tukufu inapiga marufuku kwa mtu yoyote kufanya biashara katika eneo hilo. Serikali kupitia Baraza la Mji wa anzibar itajitahidi kuliboresha eneo hilo kwa kuweka bustani ya kupumzikia wananchi kama ilivyo katika ramani ya Mipango Miji.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wale wote wanaoendelea na mtindo huu wa kulivamia eneo hilo kwa shughuli za kibiashara waache mara moja, na naziagiza taasisi zote zinazoshughulikia masuala ya biashara pamoja na utoaji wa vibali katika maeneo hayo na hata yale ya maeneo ya Ng'ambo kama vile Soko la Mwanakwerekwe kuwachukulia hatua wafanyabiashara wenye tabia hii mbaya ya kukiuka taratibu za Mipango Miji.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni dira kwetu. Hotuba hii imetusafishia na kutuonyesha njia ya wapi wananchi wa Zanzibar wanakotaka kwenda na namna gani tutawaongoza kufika huko. Tunataka kujenga Zanzibar yenye mshikamano imara ambao siku zote utajali zaidi maslahi ya jamii yetu kuliko ya mtu mmoja mmoja, vikundi vya kijamii au vyama vyetu vya siasa. Napenda kuwaasa viongozi wenzangu katika kipindi hiki cha miaka mitano tuwajibike kwa kufuata na kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya "**Maslahi ya wananchi kwanza",** na tufanye kazi kwa bidii yetu yote.

Mhe. Spika, kwa kipindi kirefu tangu tuanze mchakato wa uchaguzi hadi sasa tumekuwa tukihubiri haja ya kujenga jamii yenye maelewano, umoja na mshikamano. Takriban kampeni za vyama vyetu vyote

zilitawaliwa na wito wa kujenga Zanzibar mpya yenye mshikamano wa dhati. Hivyo, marekebisho ya miswada tuliyoijadili katika kipindi chote cha Baraza lako Tukufu ina lengo la kuhakikisha ubora wa kiwango cha utumishi pamoja na kuimarisha utawala bora. Jambo la msingi ni kuelewa kuwa yote hayo ni miongoni mwa vigezo vya kuweza kupima kiwango cha mshikamano katika jamii.

Hivyo, napenda kuwaomba viongozi wenzangu kuwa tuondoke hapa leo tukiwa na lengo moja la kutekeleza kwa vitendo ahadi zetu za kujenga mshikamano, umoja, maelewano na upendo ambao tuliwaahidi wananchi wetu na kama tulivyouonyesha ndani ya Baraza hili katika mkutano wake huu wa nane. Tuondoke hapa leo tukiwa na moyo huo huo.

Mhe. Spika, uhusiano wa uhuru na demokrasia pamoja amani na uchumi ni mambo yanayotegemeana sana. Ni mategemeo ya wananchi wengi baada ya marekebisho ya shughuli za utumishi Serikalini, wangependa kuona kuwa matokeo ya marekebisho yake yatawasaidia kuimarisha maisha yao na kuwa na matumaini zaidi. Ni matumaini yangu kuwa nyote hapa mtakubaliana nami nikisema kuwa Serikali ya awamu ya saba imekusudia kujenga uchumi imara ambao utaondokana na utegemezi kwa kutambua wazi kuwa bila ya uchumi imara amani yetu tunayojivunia hivi sasa itakuwa mashakani. Lakini kabla ya yote hayo ni muhimu kuimarisha usimamizi wa kiwango cha uwajibikaji.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka kuwa siku zote shida, maradhi na njaa hujenga hasira ambazo hatimaye huzaa machafuko ndani ya jamii. Katika kujenga uchumi imara, jitihada za Serikali kwa ushirikiano na wananchi wake ndio miongoni mwa mambo ya msingi yanayohitajika katika kujenga Taifa letu hivi sasa.

Kwa upande wangu nitajitahidi kwa uwezo wangu wote nikishirikiana na viongozi wenzangu kusimamia kazi na changamoto zinazotukabili katika azma ya kujenga maisha bora kwa wananchi wetu kwa kuongeza kiwango cha uwajibikaji ndani ya Serikali. Naomba viongozi wenzangu kutokubali kushindwa katika kusimamia azma hii kwani naamini kwa dhati kuwa tukiwa pamoja tutashinda. Kwani sote tunatambua wazi kuwa umoja ni nguvu na penye wengi haliharibiki jambo.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba nieleze machache kuhusu kadhia mbali mbali zinazolikabili Taifa letu ambazo zikiachiwa bila ya kuchukuliwa hatua madhubuti tunaweza kuhatarisha amani, umoja na

mshikamano wa nchi yetu kutokana na wananchi kukosa imani na viongozi pamoja na Serikali yao.

Mhe. Spika, moja ya kadhia hizo ni suala la ardhi. Sote tunaelewa kwamba ardhi ni uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yoyote ile. Ardhi, ikitumika vizuri kutasaidia kuleta maendeleo ya kiuchumi na hasa katika sekta za kilimo, viwanda, biashara na uwekezaji.

Mhe. Spika, **u**pimaji na ugawaji wa ardhi hauna utaratibu na utaratibu uliyowekwa baadhi ya nyakati haufuatwi. Matokeo yake nchi yetu kukumbwa na migogoro mingi ya ardhi. Hakuna hata Mkoa mmoja kati ya Mikoa yetu mitano uliokuwa salama ambao hauna migogoro ya ardhi. Kwa bahati nzuri, baadhi ya migogoro hiyo imeweza kutatuliwa kwa busara za Serikali za Mikoa. Hata hivyo, bado ipo migogoro mingi ambayo bado kutatuliwa na migogoro hii kwa bahati mbaya inawahusu wananchi wa kawaida ama kwa kuporwa au kunyang'anywa ardhi zao ambazo wamekuwa wakizitumia kwa muda mrefu kwa kujikimu wao na familia zao na hasa zile ardhi za urithi.

Mhe. Spika, naomba kutoa rai kwamba juhudi zichukuliwe kati ya walalamikaji na walalamikiwa kuimaliza migogoro yao hiyo kwa amani na salama na muafaka kupatikana baina ya pande husika. Ningeomba Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Umeme kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu kasoro hizo kwa haraka sana.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada za Serikali kukabiliana na migogoro ya ardhi na kutafuta namna ya kuitatua, natoa wito kwa Idara ya Ardhi na Upimaji kuyapima maeneo yote yanayomilikiwa kihalali na Taasisi za Serikali na kuyapatia hati ya umiliki ili kuondosha malalamiko ya baadhi ya Taasisi hizo kuvamiwa maeneo yao na wajanja wachache.

Kwa mfano, uvamizi wa maeneo yanayozunguka maskuli na vyuo mbali mbali Unguja na Pemba pamoja na kuvamiwa kwa mashamba yanayomilikiwa na Serikali. Sambamba na hilo, naiagiza Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Umeme kuwapimia wananchi maeneo yao ambao kwa muda mrefu waliomba kufanyiwa hivyo ili waweze kupatiwa hati miliki zao.

Mhe. Spika, Serikali imefanya kila jitihada kutoa viwanja kwa wananchi kwa ajili ya kujenga makaazi yao. Ni bahati mbaya

sana kwa baadhi ya wananchi kuhodhi viwanja hivyo kwa madhumuni ya kuvifanyia biashara ya kuviuza kwa bei kubwa sana, hadi kufikia Shilingi Milioni 40 – 50. Viwanja ambavyo wao walipimiwa na Serikali kwa kiasi cha shilingi 150,000/= tu. Kwa kupitia Baraza lako tukufu, Mhe. Spika, napenda kutoa onyo kwamba mtindo huo uachwe. Serikali hivi sasa itachukua hatua kwa mujibu wa sheria wa kuvirejesha Serikalini viwanja vyote vilivyopimwa na kugaiwa kwa wananchi ambavyo bado havijaendelezwa na muda wa kufanya hivyo kisheria tayari umeshapita.

Mhe. Spika, ujenzi katika maeneo ya wazi ni jambo ambalo halikubaliki. Siku chache za nyuma nilitoa onyo na leo narudia tena kusisitiza kupitia Baraza lako Tukufu kuwatanabahisha wananchi wasikubali kupimiwa au kuuziwa viwanja katika maeneo ya wazi au viwanja vya michezo. Kufanya hivyo ni kujitafutia hasara ya bure kwa jengo lolote litakalojengwa katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, suala la uharibifu wa mazingira na hasa uchimbaji wa mchanga kiholela ni tatizo jingine linalohitaji kuchukuliwa hatua za haraka. Hali ya mazingira yetu maeneo yanayochimbwa mchanga hasa Mkoa wa Kaskazini, Unguja si ya kuridhisha. Wafanyabiashara wanaochimba mchanga wamekuwa ni tatizo katika kuharibu mazingira yetu maeneo ya Donge, Kazole, Bumbwini, Kianga, Mbuzini na kwengineko. Kote huko ardhi yake imebakia mashimo tu haifai tena kwa kilimo ma maeneo hayo hayatakarabatiwa haraka.

Mhe. Spika, kwa muono wangu mtindo huu mbaya tunaoendelea nao si sahihi katika kulinda, kuhifadhi na kuyaendeleza mazingira ya maeneo yetu. Sheria za utunzaji mzuri wa mazingira zipo, ni vyema zikafuatwa ili kuinusuru nchi yetu na majanga ya uharibifu wa mazingira.
Natoa wito kwa Mamlaka zinazoshughulikia mazingira kusimamia vyema sheria za mazingira na kuwatoza faini kali wale wote wanaochimba mchanga bila kufuata sheria, ikiwa ni pamoja na kutaifishwa kwa magari yao yanayotumika kubebea mchanga huo ambao huchimbwa katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa muda mrefu imekuwa ikihamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika miradi mbali mbali ya kiuchumi. Nia ya kufanya

hivyo ni kuiwezesha Serikali yetu kufaidika na uwekezaji huo kimapato na kukuza uchumi wake. Lakini kufaidika huko siyo kwa Serikali peke yake, bali hata wananchi pia ama kimapato au kiajira. Kutokana na uhamasishaji huo wawekezaji wengi kutoka ndani na nje waliwekeza katika Sekta ya Utalii kwa kujenga Mahoteli. Mahoteli haya yalisaidia kutoa ajira kwa wananchi wetu na pia kuwawezesha kuuza bidhaa zao mbali mbali kwa mahoteli hayo ambazo zimekuwa zikitumiwa na wenye Mahoteli kuwahudumia wageni wao.

Kwa masikitiko makubwa Mhe. Spika, hoteli moja ambayo iko katika eneo la Kiwengwa, Venta Club imetelekezwa na wawekezaji wake wakiwaacha wananchi wengi kutowalipa mishahara yao na pia wale waliokuwa wanapeleka bidhaa mbali mbali kutowalipa fedha zao walizostahili. Wawekezaji hao wameacha deni la zaidi shilingi 600 Milioni. Naziagiza *ZIPA* na Kamisheni ya Utalii wawafuatilie wawekezaji wa aina hii kuwadhibiti ili tabia ya namna hiyo iachwe. Uwekezaji wa aina hii ambao siyo wa uaminifu, umewaacha wananchi wetu wamefilisika na kuwa katika hali ya umaskini badala ya kunufaika. Hivi sasa Serikali inajaribu kuona namna inavyoweza kuwasaidia wananchi hao ili waweze kulipwa madeni yao.

Mhe. Spika, kama tunavyojua maji ni uhai. Pamoja na juhudi kubwa za Serikali kuwatatulia shida ya maji wananchi wake bado maeneo mbali mbali ya nchi yetu yanakabiliwa na tatizo la maji. Bado juhudi mbali mbali zinafanyika katika kuhakikisha wananchi wetu wanapata huduma hii kwa uhakika. Nawasihi wananchi wazidi kuwa wastahmilivu wakati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imo katika jitihada za kutafuta suluhisho la kudumu juu ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, tunalo tatizo kwa baadhi ya maeneo yanakabiliwa na nguvu ndogo za umeme (*low voltage*). Ninafuraha kulieleza Baraza lako Tukufu kuwa tatizo hilo karibu litapatiwa ufumbuzi. Hivi karibuni Shirika la *JICA* la Japan litaweka "*transformer*" mbili kubwa katika Kituo cha Umeme, Saateni ili kuongeza nguvu za umeme. Aidha, Shirika hilo la *JICA* litasambaza waya mpya katika maeneo yote yenye matatizo ya nguvu ndogo ya umeme *"Voltage drop".* Kazi hizi zinatarajiwa kuanza mwezi wa Machi, 2011 na kumalizika mwezi wa Juni, 2013. Mradi ambao

utagharimu kiasi cha Dola za Kimarekani 33 Milioni chini ya msaada wa *JICA*.

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu, nachukua fursa hii kulipongeza kwa dhati Baraza lako Tukufu kwa kuendesha uchaguzi ulio huru na haki uliowezesha kukamilika kwa safu ya uongozi ndani ya Baraza letu. Kwa niaba yangu binafsi na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu napenda kuwapongeza kwa dhati kabisa. Mhe. Ali Abdalla Ali kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa araza la Wawakilishi.

Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi. Aidha Mhe. Spika, napenda kuwapongeza Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando), Mhe. Hija Hassan Hija kwa kuwachaguliwa kuwa Wajumbe wa Tumbe ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Pia napenda kumpongeza sana Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kwa kuteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Serikali katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, napenda pia kuwapongeza wale wote wagombea ambao kura zao hazikutosha mara hii, hivyo lakini wamejaribu. Mhe. Spika, kwa kumalizia napeda kukushukuru tena wewe Mhe. Spika kwa kuliongoza Baraza letu kwa umahiri mkubwa. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonyesha katika kipindi chote cha majadiliano. Nawatakia kila la kheri na safari njema ya kurejea nyumbani.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu haya sasa naomba kutoa hoja ya kuliahirisha Baraza lako Tukufu hadi tarehe 23 Machi, 2011.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba hiyo mwanana ya kuliahirisha Baraza letu na hatimae kutoa hoja kwamba Baraza hili liahirishwe hadi tarehe 23/03/2011. Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hoja hiyo basi naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubalia wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuahirisha mkutano wetu huu nafikiri katika hotuba hii Mhe. Makamo wa Pili wa Rais amezungumzia habari ya semina ya *ZANTEL* ambayo imepangwa ifanyike siku ya Jumapili tarehe 30/01/2011 pale *Ocean Paradise Resort* Kiwengwa nimeombwa nitoe taarifa kwenu Waheshimiwa Wajumbe kwamba wale wote ambao wameamua kutumia usafiri wa *ZANTEL* magari yataondoka hapa kwenye eneo letu la Baraza siku hiyo ya Jumapili tarehe 30/01/2011 mnamo saa 2:00 asubuhi kwa ajili ya kwenda kwenye semina hiyo, na semina kama tulivyoarifiwa kabla itakuwa inaanza kwenye saa 4:00 asubuhi.

Kwa hivyo, mapema tunatakiwa tufike kule na kwa maana hiyo wale ambao wanatumia usafiri wa *ZANTEL* wanaombwa waondeke hapa saa 2:00 asubuhi. Baada ya machache hayo sasa naomba niahirishe mkutano huu hadi tarehe 23/03/2011 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:35 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 23/03/2011 saa 3:00 asubuhi)